# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

# KISWAHILI

## (JARIBIO LA KCSE 1-10)

**Ili kuhimiza ubora wa kitaaluma, shule za kitaifa zinazofanya vizuri zaidi hushirikiana kwenye mkusanyiko wa mitihani ya pamoja ya "KCSE 2025 Top Schools". Lengo la juhudi hizi shirikishi ni kuwasukuma wanafunzi na kuimarisha utayari wao wa mitihani ya kitaifa kupitia matumizi ya mitihani yenye changamoto. Lengo la kushiriki rasilimali za shule na kushiriki mikakati ni kuinua ufaulu wa wanafunzi na kukuza utamaduni unaozingatia ufaulu.**

---

## UFUNGUO WA MAFANIKIO!

---


***For Marking Schemes***

***Mr Isaboke 0746 222 000 / 0742 999 000***

# MWALIMU CONSULTANCY

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 1

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**
**MUDA: SAA 1¾**

JINA……………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………

INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1. *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima**.*
2. *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
3. *Kila insha isipungue maneno **400.***
4. *Kila insha ina alama 20.*
5. *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.***
6. *Insha zote **sharti** ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa kwenye kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| Jumla | 40 | |

## MASWALI

1. Wewe ni katibu wa jopo lililochunguza sababu zinazozifanya jamii mbalimbali nchini zisiwe na maridhiano na utangamano. Andika ripoti.

2. Mtoto mvulana anakabiliwa na hatari ya kukosa kufaulu masomoni kuliko mtoto msichana katika karne hii. Fafanua.

3. Andika insha inayofafanua ukweli wa methali: Bila silaha usiingie vitani.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo: Sauti hiyo ilikuwa ya kutisha…

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 1

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA**……………………………………………………………………………………

**SHULE**………………………………………………… **SAHIHI**…………………………

**INDEX NO**……………………………………………… **NAMBARI**………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

- *Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote.*
- *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |

## 1.SEHEMU YA A UFAHAMU (15)

**Soma ufahamu huu kisha uyajibu maswali yanayofuata:**

Basi huu ni mwanzo tu *Mwanzo wa ngoma ni lele*.Huu ni mwanzo wa safari ndefu .Itachukua miaka na mikaka.Lakini msiwe na papara.Sharti mwanzo tutanabahi twaelekea wapi ndipo tuamue tutasafirije .Tahadhari na hatari ya hasira , visasi na papara pamoja na maradhi yanayozidi yote yaani maradhi ya matumaini yanayozidi uhalisia.Matumaini yaliopindukia ndiyo huwalewesha watu wakadhani watapata afueni wakizifuata pepo za siasa za chama kimoja au siasa za vyama vingi , mfumo wa soko huria au mfumo wa ukiritimba , mfumo wa utandawazi au mfumo wa kibepari , utawala wa kidekteta au utawala wa kidemokrasia na udini, ujamaa na ukomonisti na kadhalika.

Hatari kabisa ni ya kujenga nyumba ya karata.Nasema tena,tahadhari na ulevi wa ushindi .Mimi nashauri hivi ;hatua ya kwanza ya elimu si elimu ya shahada au stashahada zipatikanazo vyuoni.Elimu ya kuijielewa sisi ni nani twatoka wapi , twaelekea wapi na tutaurejeshaje utu pahali pake mahsusi toka kule mwituni kwa wanyama uliotokomea.

"Amani awe mtemi !"Umati ukadai Hapana hata kidogo.Badala yake acha amani iwe na mtemi mpya msinivishe joho ambalo si makamo yangu kulivaa," aliwaambia ."Kaeni mfikirie vyema juu ya mustakabali wenu.Nilichodhamiria mimi ni kushirikiana na ndugu yangu Madhubuti kumnyonyoa kipungu mmoja , ila sikutaka niingie pahala pake niruke juu nikijihadaa kwamba nitafika mbinguni."

Ila msikubali dhuluma .Dhuluma msikubali , ikija dhuluma tena msimlaumu mtu mwingine, jilaumini wenyewe.Jilaumini tu wenyewe .Nawakumbusha tu kwamba kuwepo mamlakani kwa mtemi Hamisi muda huu wote si kosa lake tu .Alisema Amani.Ni kosa letu sote .Ni kosa letu sote kwa kukubali dhuluma zake na udahlili wetu.Kwa kila mtawala katili kuna umma uliomruhusu ama kumpa uwezo wa kutekeleza ukatili wake.

Pia hatuwezi kuwa binadamu kamili endapo hatuoni walemavu kama wenzetu .Tutakuwa tumelemaa ulemavu mbaya zaidi kuliko ulemavu.Kauli hii ilkuwa tokeo la funzo alilojifunza Mwalimu Fasiri kutokana na amali na kalima za imani kuwaelekea Watoto wake walemavu.

**Maswali**

a)Kulingana na mwandishi ni mambo gani ambayo yafaa tujitahadharishe nayo**?** **(alama 3)**

**b)**Tambua aina za elimu katika maisha **.** **(alama3)**

**c)**Kulingana na taarifa ni mambo gani yanayochochea dhuluma katika jamii**?** **(alama 4)**

**d)**Ukirejelea kifungu hiki, eleza maana ya ngoma ni lele**.** **(alama 2)**

**e)**Binadamu kamili ana sifa gani? **(alama 1)**

**f)**Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika katika kifungu;

i)nikijihadaa nitafika mbinguni **(alama 1)**

ii)Kumnyonyoa kipungu **(alama 1)**

## 2. SEHEMU YA B. UFUPISHO (alama 15)

**Soma kifungu kisha ujibu maswali**

Ripoti za kila mara kuhusu uharibifu wa pesa za umma katika serikali za kaunti ni za kusikitisha .Kuna mabilioni ya pesa za mlipa ushuru ambazo hufujwa katika serikali kuu na hivyo basi wananchi wanakosewa sana wanapoona mtindo huu ukiendelea pia katika serikali za kaunti. Wakati katiba ilipitishwa mwaka wa 2010, Wakenya wengi walikuwa na matumaini mno kwamba ugatuzi ungewatatulia matatizo ambayo walikuwa wakiyapitia katika tawala zilizotangulia hasa katika maeneo yaliotengwa kimaendeleo.

Miaka Ishirini na mbili baadaye, kuna mafanikio yamepatikana ila hatua kubwa Zaidi inaweza kupigwa katika kuboresha Maisha ya raia kama mianya ianyotumiwa kufuja pesa za raia itazibwa. Wizi huu unajumuisha pia jinsi magavana wanavyobuni nafasi za kazi zisizo na maana ambazo wakati mwingine hutoewa kwa jamaa na marafiki wao , ni sharti ukomeshwe mara moja.

Kuna wananchi wengi ambao tayari wameanza kufa moyo kuhusu umuhimu wa ugatuzi ilhali ukwel ni kwamba hatungependa kurejelea utawala ulio chini ya serikali kuu pekee.Changamoto za ugatuzi zinazosababishwa na ulafi wa viongozi wachache zinatoa nafasi kwa wakosoaji wa mfumo wa uongozi kushawishi wananchi n ahata wahisani wasishughulike kuchangia katika maendeleo ya kaunti zao.

Juhudi zozote zile za maendeleo haziwezi kufanikishwa bila ushirikiano kutoka kwa wananchi na wahisani na hivyo basi ni jukumu la viongozi kuonyesha nia ya kutumia mamlaka walizopewa kwa manufaa ya raia. Tume ya maaddili ya kupambana na ufisadi (EACC) kufikia sasa imeonekana kufanya kazi nzuri kwa kuwasaka na kuwashtaki magavana walio mamlakani na wengine walioondoka kwa kushukiwa kufuja mali za umma.Tungependa asasi zote zinazohusika na msuala ya kupambana na uhalifu , Pamoja na wadu wengine katika jamii wenye nia njema kwa wananchi wasitambue mambo maovu yanayotendeka katika kaunti zao.

Nchi hii inatawala kwa misingi ya kisheria na hivyo basi hakuna sababu kumhurumia kiongozi yeyote anayekiuka sheria anapokuwa mamlakani kwa msingi wa mamlaka anayoyashikilia .Ni kupitia adhabu kali za kisheria pekee ambapo tutafanikiwa kukomesha uongozi mbaya kwani kama wananchi watakuwa wakisubiri kuwaadhibu wahusika kwa kuwaondoa mamlakani pekee watakuwa wametoa nafasi ya ufujaji kwa viongozi wapya kila miaka mitano.

**a)** Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 80. (Alama 8, alama 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

b)Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno 70.(alama 7, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3.SEHEMU YA C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (alama40)

**a)i)**Andika vigezo muhimu vya kuainisha konsonanti (**alama 2)**

**ii)**Tofautisha sauti zifuatazo /sh/ na /ch/ **(alama 1)**

**b)**Tumia kiimbo katika sentensi mbili tofauti sahii kudhihirisha uamilifu wake**.** **(al.2)**

c)Eleza maana za maneno yafuatayo kwa kuzingatia mahali ambapo shadda imewekwa **(alama 2)**

**'ala……………**

**A'la……………**

**d) Fafanua** dhana ya sauti mwambatano kwa kutolea mfano sahihi**.** **(alama 2)**

**e)**Bainisha majukumu ya viambishi katika kitenzi **hiki** **(alama 2)**

Nimemkimbilia

f)Weka nomino hizi katika ngeli mwafaka

i)debe**…………………… (alama1)**

ii)Mtaimbo**……………… (alama 1)**

g)Yakinisha

Mgonjwa yule hasikii wala kusema lolote**.(alama2)**

h)Andika kwa ukubwa **(alama2)**

Panya huyo alinaswa mtegoni na nyama kubwa mdomoni.

i)Geuza kauli iliyo kwenye mabano

i)Wanyama pori huwavutia watalii(tendwa**)(alama1)**

**j)**Andika katika usemi halisi **(alama3)**

Mama alitaka kujua kama kulikuwa na jamaa yake ambaye alikuwa ameugua ugonjwa huo.

**k)Tumia** kiwakilishi cha pekee chenye kuleta dhana ya msisitizo katika sentensi sahihi **(alama2)**

**l)**Changanua kwa njia ya mstari **(alama 4)**

Waswahili husema chema chajiuza ,kibaya chajitembeza.

**m)**Andika sentensi upya kulingana na maagizo **(alama2)**

Ongezeko la visa vya uhalifu linatishia kuangamiza amani katika miaka ya hivi karibuni.

**n)**Tunga sentensi moja kwa kutumia kirai kihusishi kisha uigie mstari **(alama 2)**

**o)**Bainisha vishazi

Tangu alipowasili kutoka Nairobi amewasaidia maskini wengi**.** **(alama 2)**

p)Eleza matumizi mawili ya alama ya mkato **(alama2)**

q)Onyesha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo (**alama 3)**

Wanawali walirembeshwa nyusi kwa wanja mweusi.

r)Kamilisha methali ifuatayo **(alama 1)**

Mchama ago hanyeli**…………………………………………………………………………………**

## 4.ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**a)**Taja mambo matatu yanayopelekea kufa kwa **lugha** **(alama 3)**

**b)**Isimujamii ina umuhimu gani kwa wanafunzi wa Shule ya Upili ? **(alama 4)**

**c)**Andika sifa tatu utakayotumia kuwatangazia watu kuhusu kinyang'anyiro cha soka. **(alama3)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 1

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

- *Andika jina lako, shule, nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
- *Jibu maswali manne pekee*
- *Swali la kwanza ni la lazima*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

## SEHEMU A: RIWAYA

**Clara Momanyi:** *Nguu za Jadi*

**1. Lazima**

i. "Kuna waliomwita mnyakuzi huku wengine wakimwita dudumizi kwani alinyemelea viota vya wengine. Hajengi bali hubomoa."

**a)** Jadili sifa **nne** za anayerejelewa katika dondoo. **(alama 4)**

ii. **"Karibu mwenzangu. Subiri nikuletee kikombe cha chai''**

"Hata usilete,sin a hamu ya chai mwenzangu. Nina machungu moyoni. Ndiposa nimekuja unisaidie kuyapanguza … kuyamaliza hutaweza."

**a)** Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

**b)** Fafanua umuhimu wa msemaji wa **maneno yaliyokolezwa** katika kuendeleza ploti kwenye riwaya *Nguu za Jadi*. **(alama 4)**

**c)** Eleza machungu ambayo msemaji wa maneno yaliyokolezwa anayo moyoni, ambayo angependa asaidiwe kuyapunguza katika riwaya Nguu za Jadi. **(alama 4)**

**d)** Jadili mbinu ambazo Mtemi Lesulia alizitumia kubakia uongozini ukirejelea riwaya *Nguu za Jadi*. **(alama 4)**

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**Timothy Arege:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

**2.** "Haikuwa mara moja mnavyofikiria. Ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi."

**a)** Eleza muktadha wa maneno haya. **(alama 4)**

**b)** Kwa hoja **nne**, onyesha athari ya ulevi katika maisha ya mzungumzaji. **(alama 4)**

**c)** Onyesha umuhimu **sita** wa mandhari ya dondoo hili. **(alama 6)**

**d)** Mzungumzaji ameendeleza maudhui ya mabadiliko. Thibitisha ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. **(alama 6)**

**3.** "Mtu ana ubaguzi kama nini! Ana moyo mgumu kama jiwe! Amejaliwa lakini bahili kama mchanga wa dhahabu. Hajui mali ya bahili huliwa na wadudu."

**a)** Bainisha mbinu **nne** za kimtindo zilizotumiwa katika dondoo**.** **(alama 4)**

**b)** Mzungumzaji anaashiria kwamba anayerejelewa alikuwa mchoyo. Onyesha kina cha kauli hii ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. **(alama 6)**

**c)** Jadili jinsi maudhui yafuatayo yalivyoshughulikiwa katika tamthilia *Bembea ya Maisha*. **(alama 10)**

i. Usasa
ii. Taasubi ya kiume

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.)**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 4 au 5*

**Yussuf Shoka Hamad:** *Mzimu wa Kipwerere*

**4.** "Katika kijiji hiki kuvuta kileo chochote aina ya tumbaku kulikuwa marufuku na kungeweza kugharimu hata maisha ya mtu. Vilevile, kubwia unga na hata kunywa pombe yalikuwa makosa ya jinai ingawa pamoja na juhudi zote hizi kuzuia dawa kama hizi, mji wa watawa uliongoza kwa uingizaji, usambazaji na hata utumiaji wa vileo na dawa za kulevya, ukizingatia kuwa mambo yote haya yalikuwa yamepigwa marufuku na mzimu na yalimlazimu kila mtu kuyazingatia. … hayakuwa maswali rahisi kujibika si kwa sisi tu wahenga, bali hata mzimu wetu bila shaka haukuwa na jibu!"

**a)** Fafanua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Dondoo hili limetawaliwa na mbinu **moja kuu** ya kimtindo. Itaje na uithibitishe. **(alama 2)**

**c)** Kwa hoja mwafaka, eleza jinsi suala la unafiki linavyojitokeza kwenye dondoo hili na katika hadithi nzima ya *Mzimu wa Kipwerere*. **(alama 9)**

**d)** Bainisha toni inayojitokeza katika dondoo hili. **(alama 2)**

**e)** Fafanua vigezo **vitatu** unavyoweza kuzingatia katika kutambua sifa za wahusika kwenye hadithi *Mzimu wa Kipwerere*. **(alama 3)**

**Mzamane Nhlapo:** *Nipe Nafasi*

**5.** "Jamii na serikali zinatunyima sisi wanawake uhuru.…Kabla sijafa, nataka kwanza niwe nimepata nafasi ya kuyaboresha maisha yangu na yale ya wanangu."

a) i. Taja asasi **mbili** za jamii zinazotumiwa kuwakandamiza wanawake. **(alama 2)**

**ii.** Huku ukirejelea hadithi ya *Nipe Nafasi*, fafanua jinsi jamii na serikali zimewanyima wanawake uhuru**.** **( alama 7)**

**iii.** Jadili juhudi **tano** za mzungumzaji katika kuyaboresha maisha yake na maisha ya wanawe ukirejelea hadithi *Nipe Nafasi*. **(alama 5)**

**Paul Ngángá Mutua:** *Harubu ya Maisha*

b) "Mwenyewe wajua mimi sipendi mambo ya kukopa. Isitoshe mimi nimekuja hapa likizo. Sasa zimekatika wiki mbili nawe huyo na kazi tu."

Fafanua umuhimu **sita** wa mzungumzaji wa maneno haya katika kuijenga hadithi *Harubu ya Maisha*. **(alama 6)**

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7*

**6.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***.**

Pana haja ya kupima, neno tuzowele –angu
Tusizowee kusema, hili ni teuo langu
Huenda huji mapema, -angu huja kuwa tungu
Ikaja kukusakama, na kukuposha kwa Mungu
Pana haja ya kupima.

Neno huwa ni la kwako, likiwa ndani moyoni
Lakini katu si lako, likishavuka menoni
Kwa hivyo likutokako, liweke kwenye mizani
Linaweza kuwa cheko, ama tusi kwa wendani
Pana haja ya kupima.

Vivyo hivyo kwa lebasi, huwa yako kisutuni
Hivyo nina wasiwasi, wambe yako sebuleni
Itavutiya matusi, ya wenzio insane
Wakakuchoma nafusi, kwa mishale ya lisani
Pana haja ya kupima.
Mwana ujuwe ni wako, punje ukiimezele
Lakini katu si wako, nde ukimuletele
Akiwa yu ndani yako, ni wa duniya vivile
Ukishishilia ni wako, muavye takakuole
Pana haja ya kupima.

Maisha nayo si wako, utabaradi milele
Ungayaishi ja yako, ni tunu ya maumbile
Mgawa si kufu yako, mshindane hili lile
Akupapo akupoko, utaishi palepale
Pana haja ya kupima.

Ni chetu chako si chako, ulimwengu huwa vile
Juhudi zingawa zako, wa kufaidi ni wale
Ikifika siku yako, nyono zikukae mbele
Ulichosema ni chako, huwabakiya wawale
Pana haja ya kupima.

Kaseme na moyo wako, Ubaini haya yale
Ukiambacho ni chako, kisikupe mageule
Kitu utajacho chako, huenda kiwe cha wale
Na usemacho si chako, kiwe chako ndicho kile
Pana haja ya kupima.

***Maswali***

**a)** Fafanua dhamira ya mwandishi wa shairi hili. **(alama 2)**
**b)** Pambanua bahari zozote **tatu** za shairi hili**.** **(alama 3)**
**c)** Dhihirisha kwa kutoa mifano matumizi ya uhuru wa mshairi. **(alama 6)**
**d)** Tambua toni inayojitokeza kwenye shairi hili. **(alama 2)**
**e)** Andika ubeti wa **nne** kwa lugha tutumbi. **(alama 4)**

**f)** Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi . **(alama 2)**

i. Lebasi
ii. Punje ukiimezele

**7.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*

Daima alfajiri na mapema
Hunipita na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa na jasho
Ili kujikimu kupata malisho.
Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbwiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu
Na miti yote hujipinda migongo;
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akicheka ha ha ha ha ha ha…

Na mimi hubaki nikijiuliza
Kuna siri gani inamliwaza?
Au ni kujua au kutokujua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao.
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Anayalimia matumbo ya waroho
Kuna jao gani linamridhisha?
Laiti angalijua, laiti angalijua!

**Maswali**

**a)** Fafanua hali ya mzungumzaji katika shairi hili. **(alama 5)**

**b)** Tambua aina **tatu** za taswira zinazojitokeza katika ubeti wa pili wa shairi hili. **(alama 3)**

**c)** Bainisha nafsi neni katika shairi hili. **(alama 1)**

**d)** Eleza toni ya shairi hili. **(alama 1)**

**e)** Bainisha vipengele **vinne** vya kimtindo katika shairi hili. **(alama 4)**

**f)** Pambanua muundo wa shairi hili. **(alama 4)**

**g)** Tathmini umuhimu wa maswali balagha katika shairi hili. **(alama 2)**

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

***8.*** *Soma utumgo ufuataao kisha ujibu maswali yanayofuata*

Walikuja mahasidi, ah, walikuja
Nyayo zao zikirindima, ah, rindima
Kwa ghamidha ya uadui, oh uadui
Wali wakibeba sime
Wali wakibeba mata
Wali wakibeba mienge
Ya moto kutangazia
Kwao kuwasili

Walikuja kwa ndimi
zilizohimili cheche
matusi kutumwaiya
hawakujua ya kwamba
Mbele ya mhimili huno wetu
Wao wali vipora
Kwenye mlima wa sugu,
walituvamia
Aliwakabili mbwene
Mwana wa ngwamba, ee mbwene
Aliwakabili mbwene kwa kitali kikali
Wali wametuteka ja samaki kwenye
dema
Wali wamewapukutisha
Wetu mabarobaro
Aliwakabili mbwene
Ee mbene, mwana wa ngwamba
Aliwakabili
Kwa hamasa za ujana
Kwa uchungu wa kuumbuliwa
Wa wetu wana.

Aliwakabili mbene
Nao wakalipiza shambulizi
Kwa kujidai majagina
Walijibwaga uwanjani
Laiti wangalijua wanajikabidhi
Viganjani mwa mbwene
Aliwakabili mbwene , ee
Mwana wa ngwamba, shujaa asoshindwa
Alipigana kitali
Cha kufa na kupona
Kuiopoa jamii yetu kuirejesha hadhi yetu
Kuirejesha mifugo yetu
Kuwarejeshea wakulima vikataa vyao
Kuwaokoa vipusa wetu
Nyara waliotekwa, ati walipiza kisasi
Aliwakabili mwana wa ngwamba
Aliwakabili upepo wa kusi
Hata kikomo cha mapambano kilipofika
Wagundi walijua kwamba
Walikuwa na mwana, ee mwana
Mbwene, ee mwana wa ngwamba
Hakuwa na kifani, ee kifani
Alipigana nao, ee mwana wa ngwamba
Kwa siku kumi bila tonge wala tone la maji
Kwetu kukenda kicheko cha wokovu
Kwao kukenda kilio

**Maswali**

**a)** Huu ni wimbo wa sifa. Thibitisha kwa kutolea mifano **mitatu** kifunguni. **(alama 3)**

**b)** Bainisha sifa **tatu** za jamii ya nafsineni katika utungo huu. **(alama 3)**

**c)** Huku ukitolea mifano, bainisha vipengele **vinne** vya kimtindo ambavyo nafsineni ametumia kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. **(alama 4)**

**d)** Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii yako. Fafanua hatua **nne** utakazochukua ili kuishawishi dhidi ya hali hii. **(alama 4)**

**e)** Jadili mbinu zinazoweza kutumiwa kukusanya na kuhifadhi data kuhusu vitanzandimi. **(alama 4)**

**f)** Fafanua njia **mbili** ambazo kwazo msikilizaji anaweza kuchangia katika uwasilishaji wa kipera hiki. **(alama 2)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 2

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**
**MUDA: SAA 1¾**

JINA…………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………

INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1) *Andika jina lako, nambari ya mtihani na tarehe katika karatasi ya majibu.*
2) *Karatasi hii ina maswali manne.*
3) *Jibu maswali mawili pekee. Kila swali lina alama ishirini.*
4) *Swali la kwanza ni la lazima.*
5) *Chagua swali jingine lolote kutoka kwa matatu yaliyosalia.*
6) *Majibu yote yaandikwe katika karatasi ya majibu uliyopewa.*
7) *Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.*

***Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 |
|---|---|---|---|---|
| UPEO | 20 | 20 | 20 | 20 |
| ALAMA | | | | |

| UPEO | 40 |
|---|---|
| ALAMA ZA MTAHINIWA | |

# MASWALI

**1. SWALI LA LAZIMA.**

Gari unalosafiria limehusika katika ajali mbaya barabarani. Japo kuna walioaga dunia, wewe hujadhurika kwa njia yoyote.

Andika mahojiano kati yako na mwandishi wa gazeti la Mwangaza ambaye amekuja kukuhoji kuhusu ajali hiyo.

**2.** Pendekeza njia mbalimbali zinazoweza kutumiwa ili kuleta utangamano wa kitaifa.

**3.** Sitapiki nyongo harudi haramba.

**4.** Malizia kwa maneno haya**…** hapo ndipo nilipogundua umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 2

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

***Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)***

**MAAGIZO.**

**a.** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**b.** *Jibu maswali yote kwa nafasi wazi ulizoachiwa.*

**c.** *Watahiniwa wanaweza wakaadhibiwa iwapo hawatazingatia maagizo.*

**d.** *Majibu yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MTAHINI PEKEE.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| JUMLA | | |

## 1. UFAHAMU

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Ilikuwa jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa Taarifa ya habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe pesa za kiinua mgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi lake mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki. Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, Waziri wa Kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia. name nilikuwa naanza kuumakimikia mradi huu.

Baada ya tarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichulua mara moha. Usingizi niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kilimo nilitenga ekari kumu za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nilipa shilling elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejeo. Kwanza, nililipa shilling 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunu amagunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilling 3,300 kila gunia. Mwzi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazao bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilling 1,000 kila ekari. Mvua ilinesha vizuri na baada ya siku saba mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mebgu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua wa kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilal kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo ‘amonia’. Gharama yake ikawa shilling 1,300 kila gunia. Hivyo, nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano.

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa maisha. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapita njia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siwanawaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanzi wanfu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno

nitakayopata kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa 'Usikate majani, mnyama hajauawa.'

Bila taarifa wala tahadhari mvua ikatoweka. Hayakupita majuma mawili mahinda yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahind, shamba ilkageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makasio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi yfanyavyo moshi.

Lakini 'Muumba ndiye Muumbua'. Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha.Muda si muda mahind yalianaza kunawiri. Kumbe tukio lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafu huku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba nikaona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli. Muda sio mferu mahindi yalirudi hali yake tena, kisha yakakomaa. Haraka za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli kii ikawa shilingi 5,000. Kuvuna, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. habari motomoto siku hiyo ilikuwa: "MAHIND GUNIA 900/-" Niligutuka usingizini.

## MASWALI

**(a)** Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari. **(al 1)**

**(b)** Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika? **(al 1)**

**(c)** Taja matatizo matatu yaliyotisha mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi. **(al 3)**

**(d)** Eleza maana ya methali zifuatazo: **(al 4)**

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa

(ii) Muumba ndiye muumbua

**(e)** Eleza mambo mawili yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia. **(al 2)**

**(f)** Kwa nini msimulizi alisem maumbile ni kitu cha ajabu? **(al 2)**

**(g)** Eleza maana ya: **(al 2)**

(i) kiinua mgongo

(ii) manyakanga wa kilimo

## 2 UFUPISHO (alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa

lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

**(a)** Fupisha aya ya pili na tatu **(maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**(b)** Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.

(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**a.** Taja na utofautishe irabu za mbele. **(alama 2)**

**b.** Tunga sentensi Moja kubainisha maana mbili za neno kikosi. **(alama 2)**

**c.** Andika katika wingi. **(alama 1)**

Jino langu bovu linaloniuma linanitatiza.

**d.** Tumia kielezi cha wakati badala ya kielezi kilichotumika katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Watalii walitutembelea mjini Nakuru.

**e.** Geuza sentensi zifuatazo kulingana na maagizo. **(alama 2)**

**i.** Maimuna anapika wali. (wakati uliopo hali isiyodhihirika)

**ii.** Wao walisoma riwaya hiyo. (wakati ujao hali timilifu)

**f.** Unda neno lenye muundo ufuatao. **(alama 2)**

**i.** Nafsi ya kwanza umoja.

**ii.** Hali timilifu

**iii.** Mtendewa

**iv.** Mzizi

**v.** Kauli ya kutendea

**vi.** Kauli ya kutenda/ kiishio

**g.** Tumia nomino zifuatazo za kawaida kuunda nomino za jamii. **(alama 2)**

**i.** Nzige

**ii.** Zabibu

**h.** Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno KAMA. **(alama 2)**

**i.** Kihusishi

**ii.** Kitenzi

**i.** Eleza matumizi ya neno <u>wale</u> katika sentensi hii. **(alama 3)**
Wale walioiba ni mabanati wale ambao waliambiwa wale kabla ya kitendo hicho.

**j.** Changanua kwa mstari. **(alama 4)**
Yohana na Otieno hucheza kandanda.
**k.** Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano. **(alama 3)**
**l.** Onyesha matumizi ya viwakifishi vifuatavyo katika sentensi. **(alama 2)**
i. Kibainshi
ii. Parandesi
**m.** Tumia neno –baya kama: **(alama 3)**
**i.** Kiwakilishi
**ii.** Kivumishi

**iii.** Kielezi katika sentensi
**n.** Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya A- WA. **(alama 2)**
**o.** Bainisha maana mbili ya sentensi hii. **(alama 2)**
Umu alimwandisha mkewe.
**p.** Unda nomino nne kutokana na kitenzi. **(alama 4)**
<u>Fa</u>
**q.** Geuza katika usemi halisi. **(alama 2)**
Askari jela alimuuliza Kendi kama alidhnani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja.

## 4. <u>**ISIMU JAMII**</u> **(alama 10)**

(Mdundo wa muziki) kina mama mpo…..! Kina siste nanyi… are you there? Kampuni ya platinium imewaletea mafuta mpya ya silk. Mafuta hayo yana vitamin C, Sunscreen na yana marashi ya kupendeza. Ukiyatumia kwa wiki moja tu, ngozi yako itakua laini na nyororo kama ya kitoto kichanga. Nayo macho ya wote, Waaa! Yatakuwa kwako 24/7. Jinunulie! Jinunulie! Mafuta ya silk. Mafuta ya wanawake wa kisasa.

**a.** Taja sajili iliyotumiwa hapa. **(alama 1)**
**b.** Taja sifa nne za sajili hii. **(alama 4)**
**c.** Kwa nini Wakenya wengi hupenda kuchanganya na kubadili msimbo? **(alama 5)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 2

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**
**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

***Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)***

**MAAGIZO:**

***1)*** *Jibu maswali **Manne** pekee.*
***2)*** *Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.*
***3)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
***4)*** *Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

## SEHEMU A: USHAIRI

1. **Lazima**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Piiiiiip piiip pooop poooop piiip piiip!
Ni mlio wa gari letu
Tayari kwa safari yetu
Safari ya maisha yetu; ya kutukwamua
Kutoka kwenye mikatale ya nyangumi
Nduli! Shetani! Ibilisi! Baradhuli! Punda Mgonjwa.
Yote hayatoshi
Ya kina maelezo kutoa kumhusu.

Ninakumbuka bayana
Kaski nemsi mafungulia bakari huonekana

Ila

Kaski hiyo, nemsi haikuwa
Kaski hiyo, hali mbadala
Kaski hiyo, jinamizi; tanzia
Kaski hiyo, simanzi litanda
Kaski hiyo, ubahaimu lipandwa ardhini, ikamea na kuzaa.

Ukweli ni kwamba,
Wakufunzi, wenye jukumu la kunoa wanagenzi
Mstari wa mbele walijipanga, ubahaimu kutenda.
Maswali, kwa bidii walifungasha
Tafiti wakazamia; kinga na kinga moto ukawaka.
Moto ambao ungekuja kuteketeza kizazi cha usoni.
Majibu, na tochi yalisakwa na kumiminwa akilini mwa watafutiwa
Uadilifu, teke ukapigwa, na kaburi la sahau kuzikwa.
Wakati hupo lakini; hayo kubainika mwiko yalikuwa.

Mwongo mmoja sasa umepita
Hali tenge tahani,
Vyuo vikuu na vya kiufundi
Mahafali wamimina taifani.

Akaaa!

Wahandisi, majumba yawaporomokea
Mawakili, kesi zawaponyoka; kubwa kwa dogo, jepesi kwa gumu
Majaji; haki wanajisi kisa na maana, ughushi
Matabibu na wauguzi; wateja wao jongomeo wapiga foleni
Marubani; ndege zashindana ardhini kutapakaa
Wakufunzi kuelewa wanachofanya, nadra kama wali wa daku
Mahasibu, uadilifu dirishani metokea; hesabu chenga yawapiga.
Maaskofu matumbo mbele wameweka, sadaka wafakamia.
Wanasiasa kusazwa hawajaachwa
Mstari wa mbele katika ufisadi; huku wakiendeleza ukosefu wa ajira.
Maafa, vifusi, mabaki ya ndege na garimoshi,
Utamaushi, msongo wa mawazo, tama na ubinafsi mejaa kila kukicha.

Waama! Waama! Waama!
Hakika! Hakika! Hakika!
Hali tulimo kwa kweli
Ni msiba wa kujitakia
Usokuwa na kilio?
Mwiba wa kujidunga
Usoambiwa pole?
Ni ngumi tulopiga ukutani
Na kuumiza mikonetu?

Gari letu sasa hivi, nanga imeshangóa
Uadilifu kwa hakika, mizizi inataka kukita
Ili jamii kwa kweli, najisi tufagie
Na kufutilia mbali, doa iloshamiri.
Kama si sisi, ni nani atakayemaliza ubahaimu huu?

**Odindo Adinda**: *Diwani ya Mchonyoto na Mashairi Mengine*

**a)** "Ubahaimu unaoyerejelewa una ila nyingi." Fafanua kwa mujibu wa shairi hili. **(alama 6)**
**b)** Pambanua umbo la shairi hili. **(alama 3)**
**c)** Tambua toni inayojitokeza kwenye ubeti wa **saba** wa shairi hili. **(alama 2)**
**d)** Onyesha namna mshairi alivyofanikisha mbinu zifuatazo za kimtindo:
i. Kejeli katika ubeti wa **tano** **(alama 2)**
ii. Aina za takriri **(alama 2)**
iii. Aina mbili za taswira **(alama 2)**
**e)** Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. **(alama 3)**

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**Timothy Arege**: *Bembea ya Maisha*

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.** "Gongo liliyamega maadili yake kimyakimya na taratibu uwajibikaji ukawa umemponyoka na kuteleza kama sabuni ya povu jingi na kumwacha na kisomo chake tu."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

b) Changanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

c) Jadili umuhimu wa msemaji wa kauli hii katika kujenga tamthilia *Bembea ya Maisha* ***(alama 5)***

d) Tathmini madhara ya gongo linalorejelewa kwa jamii ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. **(alama 7)**

**3.** "Tamaduni, mila na desturi zetu zinazidi kuyakubali mabadiliko. <u>Thamani ya mtoto wa kike imepanda na nafasi yake kupanuka</u>."

**a)** Thibitisha kwa hoja **kumi na mbili** maneno yaliyopigiwa mstari ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. **(alama 12)**

**b)** Eleza tamaduni, mila na desturi **nane** za jamii inayorelewa katika tamthilia *Bembea ya Maisha*. **(alama 8)**

## SEHEMU C: RIWAYA

**Clara Momanyi**: *Nguu za Jadi*

***Jibu swali la 4 au 5***

**4.** i) "Alisikia jina lake likitajwa kuwa miongoni mwa wanawake walioleta mabadiliko makubwa ya vijana nchini, hasa wa kiume."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Kwa hoja **kumi**, fafanua mchango wa mrejelewa, na wengine wa jinsia yake katika ujenzi wa jamii mpya kwenye riwaya *Nguu za Jadi*. **(alama 10)**

ii) Jadili umuhimu wa mandhari ya *Ponda Mali* katika kufanikisha **ploti** kwenye riwaya *Nguu za Jadi.* **(alama 6)**

**5.** "… <u>hawakujali kuwa haki ndiyo inayoinua taifa</u>. Kwamba johari hii ikiadimika, basi taifa liko hatarini. **Matuo ilikuwa ikididimizwa taratibu na wanaoabudu ukunguni**. Laiti wangalichagua jina jema kuliko mali nyingi!"

**a)** Tambua toni inayojitokeza katika dondoo hili. **(alama 2)**

**b)** Thibitisha ukweli wa kauli iliyokolezwa, kwa hoja **kumi**, ukirejelea riwaya *Nguu za Jadi.* **(alama 10)**

**c)** Onyesha mbinu ya kimtindo inayojitokeza katika kauli iliyopigiwa mstari inavyotumika katika riwaya *Nguu za Jadi.* **(alama 8)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.)**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au 7*

**Winnie Nyaruri Ogenche:** *Sabina*

**6)** i) **Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu**. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame."

a) Pambanua aina **nne** za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 4)**

b) Thibitisha ukweli wa kauli iliyokolezwa kwa mujibu wa hadithi *Sabina*. **(alama 8)**

**Dominic Maina Oigo:** *Kifo cha Suluhu*

ii) Jadili umuhimu wa barua ya Bi. Suluhu kwa Bwana Suluhu katika kufanikisha hadithi *Kifo cha Suluhu*. **(alama 8)**

**Douglas Ogutu:** *Toba ya Kalia*

**7)** i) "Kila mzazi humtakia mwanawe mema ila wakati mwingine hutumia mbinu mbovu."

Fafanua madhara ya mbinu kuu iliyotumiwa na warejelewa kumfikisha msemaji katika kilele cha ufanisi ukirejelea hadithi *Toba ya Kalia.* **(alama 7)**

**Mzamane Nhlapo:** *Nipe Nafasi*

ii) "Kabla sijafa, nataka kwanza niwe nimepata nafasi ya kuyaboresha maisha yangu na yale ya wanangu."

Onyesha vikwazo **saba** vinavyolemaza juhudi za msemaji na wenzake za kutekeleza kauli hii ukirejelea hadithi *Nipe Nafasi*. **(alama 7)**

**Phibbian Muthama:** *Nilitamani*

iii) "Nilikuwa na tumaini, naamini japo kwa kiasi fulani nilitamani na kutaka. Nilipanda ngazi kutoka kutamani na kuanza kutaka."

**"Tamaa mbele mauti nyuma."** Thibitisha kauli hii kwa hoja **sita** kwa mujibu wa hadithi *Nilitamani*. **(alama 6)**

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

***8) Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali yanayofuata.***

"Kama kesho itapambauka
Jua la kinjano kuchomoza
Kuangazia siku mpya
Siku iso tumaini
Siku bila mimi na mama mtu
Kumbuka ewe kipenzi
Usiache chozi kufurika
Kiyeyusha makini yako inuka, mwanangu inuka
Silie daima, yote tatengenea."

Mpenzi mama ulolala usingizi usio na mzindushi
Nalikumbuka vyema hili ni beti uloniandikia
Kitandani ukiwa, ukiuguza donda
Donda walokusababishia walimwengu mahasidi
Ela nataka ujue, kamwe yote si shwari kwa mlezi kikembe
Hayawezi tengenea kwa yatima alozungukwa
Na waja wenye tamaa kila kitu kurithi
Hayawezi kuwa shwari kumtaza mwenzio,
    Ulotwambia tumwite baba na kumstahi
    Ati ni amri ya Muumba.
Akitoka na muhebi, pumbao apate yeye
Wafurahia ulochuma wewe.
Najitahidi mpenzi mama
Ukakamavu kujipa
Machozi kuyafuta
Ela hino kumbuka
Kuondoka kwako huko
Hatukukutarajia, japo hukuisha kunikumbusha
Ziraili liliingia ja mwewe
Na kukwiba mithili ya kifaranga
Mama yake akitazama.

***Maswali:***

**a)** i. Ainisha utungo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. **(alama 1)**

ii. Fafanua sababu **tano** zinazothibitisha jibu lako katika swali la a (i). **(alama 5)**

**b)** Bainisha sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa katika utungo huu. **(alama 2)**

**c)** Tambua toni utakayotumia katika uwasilishaji wa kipera hiki. **(alama 2)**

**d)** Unanuia kutumia mbinu ya kushiriki katika utafiti wa kipera hiki. Pambanua manufaa ya kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

**e)** Jadili jinsi viziada lugha vinatumiwa katika kukuza vipera mbalimbali vya fasihi simulizi shuleni mwako. **(alama 5)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 3

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

JINA…………………………………………………………………………………

SHULE…………………………………………… SAHIHI…………………………

INDEX NO……………………………………… NAMBARI………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

- *Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.*
- *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
- *Kila insha isipungue maneno **400**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | TUZO |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |
| 4 | |
| JUMLA | |

## SWALI LA LAZIMA

1. Kumetokea shambulizi la kigaidi katika nchi jirani Somalia. Wewe kama balozi mwandikie raisi wa Kenya na watu wa nchi hiyo risala ya rambirambi.

2. Dhuluma dhidi ya wanawake imekita mizizi ndini. Jadili.

3. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.

4. **…**Na huo ndio ukawa mwanzo mpya.

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 3

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO……………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

***Maagizo***

**1.** Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

**2.** Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

**3.** Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| UFUPISHO | 15 | |
| SARUFI | 40 | |
| ISIMU JAMII | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

## UFAHAMU (ALAMA 15)

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekena baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya koindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulani mahususi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilkikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi uweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au

msusi untambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na "uhusiano wa chembe chembe". Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa na kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwezake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza nji: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni w aaina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

**(a)** Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. **(al 1)**

**(b)** Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. **(al 1)**

**(c)** Fafanua athari ya technolojia kwenye mahusiano ya watu. **(al 2)**

**(d)** Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. **(al 4)**

**(e)** Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. **(al 2)**

**(f)** Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? **(al 2)**

**(g)** Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(al 3)**

(i) inasigana…………………………………………………………………………………

(ii) yameghoshi………………………………………………………………………………

(iii)vighairi…………………………………………………………………………………...

## UFUPISHO (ALAMA 15)

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lililolowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhanaya "ujambazi" tena "wa kimataifa". Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi w anchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambaz ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni watakaburi hao, ujambazi ni wa watu 'washenzi' wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi peke wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevya uliosababishwa na vinyagarika kutoka nchi hizo maaluni za "ulimwengu wa tatu". Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya

kusawasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kushambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe lo lote la dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima, aliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha na Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ulizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

**MASWALI**

**(a)** Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**(b)** Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11, 2001. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**(a)** Silabi ni nini? **(al 2)**

**(b)** Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. **(al 2)**

(i) igwa

(ii) Oa

**(c)** Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. **(al 2)**

(i) Galagala ………………………………………………………………………………

(ii) Teketeza ……………………………………………………………………………...

**(d)** Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. **(al 2)**

(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa

**(ii)** Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

**(e)** Eleza matumizi ya kihusishi <u>kwa</u> katika sentensi ifuatayo. **(al 2)**

Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.

**(f)** Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. **(al 2)**

Siji.

**(g)** Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. **(al 1)**

Tepetevu

**(h)** Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. **(al 2)**

Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme

**(i)** Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. **(al 2)**

Mzalendo amemwandikia mhariri barua.

**(j)** Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. **(al 2)**

Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani

**(k)** Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. **(al 2)**

Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

**(l)** Kanusha sentensi ifuatayo. **(al 2)**

Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo

**(m)** Andika katika wingi. **(al 2)**

Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.

**(n)** Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. **(al 1)**

Mhalifu huyu <u>alitunga</u> mimba

**(o)** Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. **(al 1)**

Jua limekuwa likiwaka tangu Januari

**(p)** Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: **(al 1)**

Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga

**(q)** Akifisha sentensi hii: **(al 2)**

Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo

**(r)** Badilisha katika usemi wa taarifa: **(al 2)**

"Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi," afisa wa usalama akasem.

**(s)** Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. **(al 1)**

Aliyerembesha <u>uso</u> kwa poda.

**(t)** Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: **(al 3)**

Mwalimu amempigia wanafunzi simu

**(u)** Silabi mwambatano ni nini? **(al 1)**

**(v)** Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: <u>Rudi</u> **(al 1)**

**(w)** Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. **(al 2)**

Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.

## <u>ISIMU JAMII</u>

Maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na chagamoto tele. Fafanua zozote tano. **(al 10)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 3

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**
**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

1) *Jibu maswali **Manne** pekee.*
2) *Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.*
3) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
4) *Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

## SEHEMU A: RIWAYA

### Clara Momanyi: Nguu za Jadi

**1. Lazima**

"Pole kaka, huu ndio ulimwengu wetu… ulimwengu unaoendeshwa na sarafu, ndugu. Tumekuwa kama wanyama wa mwitu. N'ambie tofauti i wapi yakhe? Kama wanyama, hatuna tena mipaka ya umri, nasaba au vyeo."

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Fafanua maana ya kitamathali kwenye kauli iliyopigiwa mstari. **(alama 2)**

**c)** Onyesha jinsi unyama wa msemaji kwenye dondoo ulivyoathiri wengine kwenye jamii. **(alama 6)**

**d)** Kando na msemaji wa dondoo hili, kuna wahusika wengine walioendeleza utovu wa maadili katika jamii. Thibitisha. **(alama 8)**

## SEHEMU B: TAMTHILIA

### T. AREGE: *Bembea ya Maisha*

**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** Si neno mama! (Kimya.) Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi. Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Bainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c) Fafanua sifa za msemaji. **(alama 6)**

(d) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. **(alama 6)**

**3(a)** "Ndiyo ni mgonjwa lakini mume ambaye ni mwanamume kweli hangoji kuelezwa kinafanyika nini."

(i) Bainisha maudhui yanayojitokeza katika dondoo. **(alama 1)**

(ii) Onyesha jinsi maudhui uliyotaja katika (i) yalivyoshughulikiwa katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*. **(alama 9)**

**3(b)** Ndoa ni bembea. Jadili kwa kurejelea tamthilia ya ***Bembea ya Maisha***. **(alama 10)**

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

### D.M. Lutomia na P. Muthama (Wah.): *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. Yussuf Shoka Hamad**: "***Mzimu wa Kipwerere!***"

"Vipi kuhusu usambazaji wa mizigo? Tunahitaji akina mama zaidi maana mzigo ndio kama unavyouona na umejaa humu na hauuzwi kwa wingi! Umelifikiriaje hili?

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Bainisha mbinu **tatu** za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 3)**

**c)** Eleza sifa **sita** za msemaji katika dondoo hili. **(alama 6)**

**d)** Suala la dawa za kulevya limejitokeza katika hadithi, "***Mzimu wa Kipwerere***." Thibitisha. **(alama 7)**

**5. (a) "**Kwa muda wote tuliokaa pamoja, sikufichua siri yoyote ambayo nilijua". Onyesha siri ambazo msemaji hakufichua katika hadithi, "***Kifo cha Suluhu***". **(alama 7)**

(b) "Ni wajibu wetu wanawake kutetea maisha yetu na yale ya Watoto wetu." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi, "***Nipe Nafasi."*** **(alama 13)**

## SEHEMU D: USHAIRI

**Jibu swali la 6 au 7**

***6. Soma mashairi yafuatayo kisha uyajibu maswali yanayofuata***

**Shairi 1**

### MIMBA ZA MAPEMA

Zanikosesha amani, hizi mimba za mapema
Hunizushia huzuni, nikakosa kuungama
Ela leo nabaini, munisikilize vyema
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Ni ubaya wa malezi, wakwa baba au mama
Kwa kushindwa uongozi, kuongoza palo pema
Wakawaacha ja mbuzi,ndio haya huja nyuma
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Mwana avaa vibaya, nguo zisizo heshima
Nanyi mwamuangaliya, munashindwa kumsema
Tena munamteteya, haki sawa mwalalama
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Wazazi haki wandani, wengi wao sio wema
Wajivalia vimini, banati wakitizama
Ndugu hili liacheni, mimba ndio zitakoma
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Au yuwataka pipi, kama ilo na Halima
Nae ajihisi hapi, yuwaonewa huruma
Wamgomea humpi, aenda pewa na Rama
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Mara aja na rafiki, wakiume wakisoma
Kuulizia hutaki, wawacha wakinguruma
Wallahi halikomeki, mimba zitazidi vuma
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Yuwakuaga mtoto, enda kesha kwenye ngoma
Nawe huoni uzito, wampa na darahima
Ela mwisho ni majuto, eleweni wanadama
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Jengine lililo sumu, silifichi nalisema
Na ndio lashika zamu, linaloharibu uma
Mwana kumwachia simu, na shule hajakhitima
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Hata shida za nyumbani, kukosekanapo sima
Mlo ukawa jioni, wali usio na nyama
Hapo tupo hatarini, tujitumeni kwa hima
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Hizi ni beti a'shari, ndio mwisho kaditama
Nalighaliki shairi, sisemi tena kalima
Ela niloyadhukuri, yatwalieni muhima
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

**Shairi 2**
Hata nijaze dhahabu, lifurike kontena,kisha ifanye kilima
Eti nataka karibu, ya kuwa italingana,alonitendea mama
Takuwa najiadhibu, najisumbua naona,dharau zaniandama
Sitolipa masahibu, na madhila mengi sana,yalompita mama

Hata nijenge benki, kubwa kuzishinda zote,zilojengwa duniani
Pesa nijaze lukuki, kila aina apate,za ndani na za kigeni
Riyale kwake si dhiki, dirham zisikate, na Dola za Marekani
Hazitalipa mikiki, mama yangu aipate, sekunde nimo tumboni
Hata nijenge nyumba, ya ghorofa hamsini, karibu kugusa mbingu
Yenye idadi ya nyumba, alfu u thamanini, milki ya Mama yangu
Awe mwenyewe atamba,  nyumbani na sebuleni, kwa sofa ziso mbingu
Na masifa ya kujipamba, si kitu chenye thamani, ja bega la mama yangu

Hata ndege ninunuwe, Miele angani iko, na mama aishi humo
Katu chini isituwe,  kugusa chini mwiko, kila kitu kimo
Anapotaka mwenyewe, aone kule aliko, darubini ndani imo
Mwenyewe nikusumbuwe, si sawa na ubeleko, wa mama mwenye makamo

Hata nijenge mabwawa, makubwa ya kwogelea, kwa mama nimeyaweka
Maji moto yanatiwa, na baridi kila saa, aoga anayotaka
Taulo amepangiwa, sabuni za kunukia, kila chini zinatoka
Kote ni kujisumbuwa, sudusi sijafikia, kinyesi changu kunyika

Hata nitunge shairi, niwe mimi nalighani, mama atakapolala
Sauti ile nzuri, kutoa nyoka pangoni, si ya debe yenye ila
Nikawa nalikariri, mama yuko kitandani, chombezo limetawala
Haijawa ni kadiri, na yako yasi mizani, kutaka mimi kulala

Hata nipewe na vyeo, vishindavyo vyeo vyote, maarufu duniani
Na watu wanionao, heshima kwa nipate, nalindwa sionekani
Ulinzi nilionao, saa na dakika zote, vifaru komando ndani
Si sawa na chake cheo,cha mama kwa hali zote,kwake ni kuruti duni

**Maswali**

a) Linganisha na ulinganue muundo wa shairi 1 na shairi 2. **( alama 4)**
b) Linganua bahari za shairi 1 na shairi 2. **( alama 2)**
c) Kwa kutolea mifano mwafaka,eleza sababu za mshairi kutumia uhuru wake katika shairi 1. **( alama 4)**
d) Tambua nafsinenewa katika shairi 1 **( alama 2)**
e) Kwa mujibu wa shairi 1, mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja tatu. **( alama 3)**
f) Andika ubeti wa tatu katika shairi 1 kwa lugha nathari. **( alama 4)**
g) Eleza maana ya neno "**banati**" kama lilivyotumika katika shairi 1. **( alama 1)**

**AU**

***7. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata***

Baada ya mtihani yetu ya mwisho

Tulijikusanya gwarideni kuskia neno la mwisho.

Nyuso zetu zilijawa na furaha

isiyo na kifani,

Hatukujua ni ufunuo wa dunia gizani

Ni miaka tatu sasa bado sijajiunga chuo kikuu
Kisa ni matokeo yangu na wazazi kukosa ka kituu
Ni uchungu sana ila napambania kuipata nafuu

Zile ndoto zangu za kuwa rubani
Niliziwacha mkononi mwa rabani
Wale wanafunzi nilokuwa nao shuleni
Cha ajabu atusemezani kama zamani

Natamani kurudi shuleni
Ila ni tamu izi mapeni
Kwaheri mwalimu
Wewe ni mtu muhimu

**<u>Maswali</u>**

a) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru. **( alama 3)**

b) Kwa nini nafsineni hajajiunga na chuo kikuu? **( alama 2)**

c) Tetea ukweli kuwa kifungu hiki ni shairi. **( alama 4)**

d) Tambua kinaya kinachojitokeza katika ubeti wa pili. **( alama 1)**

e) Tambua mstari mshata na mstari toshelezi inayojitokeza katika shairi hili. **( alama 2)**

g) Eleza maudhui yanayotawala shairi hili. **( alama 2)**

h) Eleza aina zozote mbili za urudiaji katika shairi hili. **( alama 2)**

i) Tambua idhini moja ya kishairi katika shairi hili. **( alama 2)**

j) Eleza vipengele vifuatavyo vya kimtindo kama vilivyotumika katika shairi hili. **( alama 2)**

i) taswira

ii) sitiari

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (Alama 20)**

**8.** ***Tazama picha ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***



**a)** Tambulisha kipera kinachodhihirika hapa juu kwenye picha. **(Alama 1)**
**b)** Kipera hiki hupatikana kwenye utanzu gani. **(Alama 1)**
**c)** Kwa nini jamii inadhamini kipera hiki? **(Alama 5)**
**d)** Utanzu uliotaja kwenye b) unahitaji fanani mwenye wasifu upi kuuwasilisha? **(Alama 5)**
**e)** Umepanga kwenda nyanjani kukusanya data ya kipera hiki. Kwa nini njia ya kurekodi kwa video itakuwa bora? **(Alama 5)**
**f)** Kupitia kipera kilichotajwa katika a) hapa juu, ni shughuli zipi za kijamii zinaweza kudhihirika kipera kinapowasiliswa? **(Alama 3)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 4

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… NAMBARI………………………**

***Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)***

**MAAGIZO**

**1.** *Andika Insha Mbili. Insha Ya Kwanza Ni Lazima.*
**2.** *Kisha Chagua Insha Nyingine Moja Kati Ya Hizo Tatu Zilizobaki.*
**3.** *Kila Insha Isipungue Maneno Mia Nne. 400*
**4.** *Kila Insha Ina Alama Ishirini. 20*
**5.** *Kila Insha Lazima Iandikwe Kwa Lugha Ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

## MASWALI

**1. LAZIMA**

Mwandikie barua mhariri wa Gazeti la Baraka ukimweleza sababu za watoto wengi katika kaunti yako kuacha shule na kujiingiza katika ajira za mapema.

**2.** Vipakatalishi vimeleta manufaa mengi nchini .
Fafanua.

**3.** Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali:
Mcheka kilema hafi bila kumpata.

**4.** Andika kisa kitakachoanzia kwa maneno yafuatayo:
Kushoto kulikuwa na jitu la miraba minne ambalo lilitema cheche za matusi ungedhania ni karakana **…**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 4

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. *Andika jina lako, shule na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
2. *Andika tarehe ya mtihani na utie sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
3. *Jibu maswali yote.*
4. *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa baada ya kila swali katika kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 UFAHAMU | 15 | |
| 2 UFUPISHO | 15 | |
| 3 MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| 4 ISIMU JAMII | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (alama 15)**

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali</u>***

"Swala la idadi kubwa ya watoto wadogo wanaoendelea kumiminika mijini na kuonekana wakiranaranda mijini ovyo,halijapewa umuhimu wowote wa haja na serikali za nchi nyingi,licha ya mijadala katika warsha anuwai,zilizofanyika kujadili swala hili nyeti.

Kwa kutokuwa na sheria ama sera iliyo wazi kuhusu haki na usalama wa watoto,sarikali zetu hazina budi kukubali kubeba uzito wote wa lawama. Hii ni kwa sababu, serikali zetu zimelipuuza na kuvalia miwani swala hili kwa kuchukulia kuwa litapotea lenyewe katika hewa yabisi. Yafaa ifahamike kuwa usalama wetu katika siku zijazo utategemea jinsi tutakavyolikabili ana kwa ana tatizo hili wakati huu. Wakati wa kutenda ni sasa. Aidha, watoto hawa wanaokulia mitaani bila malezi,maelekezo wala mwongozo mwafaka wa kimaisha, wanakua bila mapenzi hivyo hawajui maana ya kupenda. Wanachokijua ni chuki na haja ya kulipiza kisasi didhi ya jamii iliyowachonga jinsi walivyo. Hawajali lolote hata kifo. Wako tayari kujikabidhi kwa haini yeyote mwenye nia mbaya,bila kujali matokeo, muradi tu, wapate riziki.

Tunapendekeza kwa serikali, washika dau kama vile mashirika ya kujitolea, viongozi wa dini, shule, vyuo na wananchi kwa jumla wachange bia katika kutafuta mikakati ya kulitatua tatizo hili kabla halijageuka kuwa janga la kijamii ambalo tutashindwa kulimudu. Mpango wa vijana hawa kujiunga na huduma ya taifa ni jambo linalofaa kutiliwa maanani.

Tunapendekeza makao Zaidi ya watoto wanaozurura mijini yajengwe ambapo watapata mafunzo ya kiufundi yatakayowawezesha kujitegemea maishani. Badala ya kulitegea mgongo swala hili, serikali zinawajibika kuwasajili hawa watoto ili waweze kuunganishwa na familia na koo zao. Utafiti uliofanywa na wataalamu wa Elimu jamii umebainisha kuwa ni asilimia kumi tu ya watoto hawa wa mitaani wasiokuwa na mahali wawezapo kupaita nyumbani. Asilimia tisini iliyobaki, angalau wana mahali wanapoweza kupaita nyumbani ilhali wanaendelea kuwa mitaani. Wazazi tumesahau wajibu wetu. Wengi wetu tumelikimbia jukumu la ulezi tulilopewa na muumba. Hawa waliojipaka masizi mwilin mzima, wanaozurura ovyo mitaani, si matokeo ya maumbile;hawakuja duniani kwa sadfa, hawakuulizwa wala kushauriwa. Makosa ni yetu wazazi. Tuliwaleta hapa duniani, kisha tukawakimbia.Hatutasamehewa duniani na akhera.

Mwenye njaa hana miiko. Ili kijiruzuku, hawa watoto daima wanachumia jaani.Kwa kudura ya jalia, huenda siku moja watalia kivulini. Asiyekuwa na wake ana mungu.Aghalabu, watoto wanaozurura mitaani hupewa pesa na wafadhili. Wakati mwingine wanaiba. Maisha haya ya kuomba au kuiba wanaona yanaridhisha Zaidi kuliko kumenyeka na kazi ya kibarua kutwa kucha. Kwa bahati mbaya, watoto hawa wamatumia pesa wanazopata kutoka kwa wafadhili kujichimbia kaburi. Aidha pesa wanazopatiwa watoto hawa wanazitumia kununulia gundi badala ya chakula.

Wafadhili wanashauriwa wawape chakula hawa watoto badala ya pesa taslimu. Kusema kweli, unapompa mtoto wa mitaani pesa,utakuwa unainua biashara ya mwenye kiwanda cha gundi,jambo ambalo litakuwa sawa na kuweka sahihi mkataba wa kifo cha mtoto mwenyewe.

Wataalamu wa afya wanaonya kuwa gundi ikivutwa kwa muda mrefu inaweza kusababisha upofu au kifo.Wataalamu hawa wanazidi kutuarifu kuwa matumizi ya muda mrefu ya gundi huathiri ubongo,figo na maini. Mtumiaji pia anaweza kupoteza uwezo wa kutembea na hata kupooza kabisa.

Sababu wanazotoa hawa watoto ni kwamba, uvutaji gundi,huwaondolea njaa,baridi ya usiku na kuwatuliza mawazo. Ni jambo la kusikitisha kwamba tunaendelea kushuhudia bila kujali hawa watoto ambao ni kiungo cha jamii yetu,wakijiangamiza. Wananchi kwa ujumla hawaha budi kuhamasishwa dhidhi ya athari ya matumizi ya gundi.Wafanya biashara wanaowauzia watoto hawa gundi yafaa wakome,la sivyo wachukuliwe hatua.Kutolitatua tatizo hili la watoto wa mitaani hivi sasa,kutapeleka kuwako kwa kizazi cha mitaani ambacho kitazaliwa mitaani,kulelewa mitaani,kuoa mitaani na kufia mitaani.Kadiri mataifa yanavyoendelea kujitia hamnazo kuhusiana na swala hili,ndivyo tunavyokubalia jinai itawale,sasa na wakati ujao.

Hawa watoto watakapokua,watageuka kuwa wapigaji watu kabari,majambazi,wezi wa kutumia nguvu ama watatumiwa na mahaini kutimiza uhaini wao.Hawa watoto wenye njaa,watalazimika hatimaye,kuwatoa wenywe shibe tonge mdomoni.Matokeo ya hali hii ni kwamba katika siku zijazo,hawa ndio watu watakaotunyima starehe ya kulala unono.Watatuchafya mitaani,majumbani,vijijini na kutuvizia mabarabarani.Tuna sababu nzuri ya kutiwa hofu na tatizo hili,kwani jinsi kizazi kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu."

## MASWALI

**(a)**Taja jambo moja linalochangia kuweko kwa watoto wanaorandaranda mitaani. **(alama 1)**

**(b)** Maisha ya mitaani huathirije watoto? **( alama 3)**

**(c)**Tatizo la watoto wanaorandaranda mitaani laweza kutatuliwaje? **(alama 3)**

(d) Eleza maana ya**:** **(alama 2)**

**i.** Hawa watoto wanachumia jaani

**ii.** Jinsi kizazi cha mitaani kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu. **(alama 2)**

iii. Mwenye njaa hana miiko. **(alama 2)**

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye taaria: **(alama 2)**

i. Aidha:

ii. Gundi:

**2.UFUPISHO:(ALAMA 15)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo***

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona

ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

**a)** Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho

(Maneno 30) (alama 5 utiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**(a)** Toa mifano miwili miwili **ya** **(al.2)**

i. Sauti ghuna ambazo ni vipasuo …………………………………………….…………..

ii. Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo ……………………………………….……………

(b) Onyehsa mofimu katika neno Aliyemcha **(al.2)**

(c) Andika sentensi yenye muundo ufuatao **(al.2)**

KN(W+V) + KT (t +RH)

**(d)** Tumia neno shirika kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja **(al.2)**

**(e)** Kwa kutunga sentensi vumisha nomino nguruwe kuwa kivumishi cha idadi bainifu. **(al.1)**

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendewa **(al.1)**

Mtoto wa waziri amekufa

**(g)** Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi **(al.2)**

Msomi hakutuzwa siku hiyo

**(h)** Tunga sentensi moja inayobainisha maana mbili tofauti za neno chuma **(al.2)**

(i) Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo. **(al.4)**

Mwalimu mkuu hupigiwa nguo pasi na Maria

(j) Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kirai nomino **(al.2)**

**(k)** Andika sentensi ifuatayo kwa **wingi** **(al.2)**

Mgeni huyo na mwingine walikula wali kwa uma

**(l)** Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja **(al.1)**

**(m)** Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika udogo **wingi** **(al.2)**

Ng'ombe wangu ana ndama mdogo

**(n)** Tunga sentensi zenye mipangilio ifuatayo; **(al.4)**

**i.** Kishazi tegemezi na kishazi huru

**ii**. Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi

(o) Eleza matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo**:** **(al.3)**

Nyamunga na kitoto wamekuwa wakila, wakiimba kikasuku

**(p)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi**.** **(al.4)**

Mtoto wa mjomba alikuja kwetu nyumbani jana

(q) Andika kwa msemo wa taarifa**.** **(al.2)**

'Yafaa tumwendee mama mkubwa ili atushauri juu ya jambo hili,' Amina alipendekeza.

**(r)** Andika kinyume cha: **(al.1)**

Chakula hiki kitamu nitakimeza

(s) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo**.** **(al.2)**

(i) Kiwakilishi nafsi huru

(ii) Kiwakilishi nafsi kiambata

**4. <u>ISIMUJAMII</u> (alama10)**

(a) Tofautisha kati ya kuhamisha msimbo na kuchanganya msimbo. **(alama 2)**

(b) Taja mambo mawili yanayochangia katika uhamishaji msimbo. **(alama 2)**

(c ) Taja kaida mbili zinazotawala maamkizi katika jamii huku ukitoa mifano mwafaka.**(alama2)**

(d) Fananisha sifa zozote nne za sajili ya maabadini na mahakamani. **(alama 4)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 4

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

***a)*** *Jibu maswali* ***Manne*** *pekee.*
***b)*** *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***Lazima****.*
***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
***d)*** *Usijibu maswali* ***Mawili*** *kutoka* ***Sehemu moja****.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU A: RIWAYA**

**Clara Momanyi: Nguu za jadi**

**1. LAZIMA.**

"<u>Dunia ni tambara bovu</u> ... bovu sana. Ukivuta utachana. Acha waende zao."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. **(alama2)**

c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(alama4)**

d) Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kutumia mifano kumi maridhawa riwayani. **(alama10)**

**SEHEMU B : TAMTHILIA**

**T.M Arege : Bembea ya Maisha**

**Jibu swali la 2 au la 3.**

**2.** Hayo ni ya kale ... na ya kale hayanuki. Wengi hawafuati tena mila hizo. Walimwengu sasa wanavaa sare moja.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

b) Fafanua tamathali mbili za usemi zilizotumika katika dondoo hili. **(alama2)**

c) Eleza sifa za mzungumzaji wa kauli hii. **(alama5)**

d) Jadili namna mila na tamaduni za Kiafrika zilivyomkandamiza mwanamke kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama9)**

Au

**3.** "<u>Bila yeye chombo kingezama</u>. Ni kwamba siwezi kumwambia haya maana atajishaua."

a) Kwa kutumia hoja tano, fafanua umuhimu wa mnenaji wa kauli hii katika kujenga tamthilia ya "Bembea ya Maisha" **(alama5)**

b) Fafanua madhara ya taasubi ya kiume katika jamii kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama7)**

c) Kwa kutumia hoja nane, tathmini ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kuzingatia mrejelewa na watu wa jinsia yake. **(alama8)**

**SEHEMU YA C: HADITHI FUPI**

**D.M Lutomia na P. Muthama (wah) : Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine.**

**Jibu swali la 4 au la 5.**

**Dominic Maina Oigo: "Kifo Cha Suluhu."**

**4.** "Mume wangu, hebu zivute fikra zako miaka kumi na mitano iliyopita tulipoingia katika mkataba wa ndoa. Kwa nini unataka kujitia hamnazo kuhusu ahadi ulizozitoa? Umesahau namna tulivyohangaika, tukachekwa na watu, tukakosa hata marafiki na hatimaye tukabandikwa majina ya ajabu? Umesahau mume wangu? Umesahau namna kazi yako ya kuuza makaa ilivyofikia hatima ya ghafla baada ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrau? Naomba ukumbuke. Ninaamini huenda umesahau! Ama cheo chako cha ubunge ulichokipata kwa mbinu nizijuazo mimi kimekulevya na kukufanya uisahau familia yako?

a.(i) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama6)**

ii) Fafanua umuhimu wa ujumbe aliotoa mnenaji wa maneno haya kwa kutumia hoja saba. **(alama7)**

b) Kwa kutumia hoja <u>saba</u>, Jadili namna suala la dhuluma lilivyoshughulikiwa katika hadithi ya Sabina. **(alama7)**

Au

**NIPE NAFASI: MZAMANE NHLAPO**

5. "... Wanaume katika nyumba ile hawatulii. Walihisi kuwa mama alikuwa amewatusi na bila shaka kuna wale waliotamani wangekuwa na nafasi, wasingechelea kumtia mkononi na kumrudi vilivyo."

a(i)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

ii) Taja suala kuu linalojitokeza katika dondoo. **(alama1)**

iii)Fafanua umuhimu wa usimulizi katika hadithi hii. **(alama8)**

b) Kwa kurejelea hadithi "Toba ya Kalia" Jadili changamoto zinazokabili mayatima.**(alama7**)

**USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7 .**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**.

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali
Ubavuni umuweke, umtowe kule mbali
Maskanini afike, umtindie fahali
Utamu anufaike, sima, bada au wali
Hatimaye ateuke, kwa viliwa vya samli
Mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyaungika
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika
Mara atakusahau, wema wako kafukia

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie
Amani yako umpeo, fanaka uirajue
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue
Ndio wake mwelekeo, yuauma avuvie
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema
Binadamu takudhili, dhili zako kazitema
Licha ya zote jamili, mwanadamu si muema
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

**Maswali**

a) Shairi hili ni la aina gani? Fafanua jibu lako. **(alama2)**

b) Eleza usaliti unaoendelezwa na mwanadamu kwa mjibu wa shairi hili. **(alama4)**

c) Tia shairi hili katika bahari tatu tofauti kwa kuzingatia; **(alama3)**

i) Mpangilio wa maneno

ii) Mpangilio wa vina

iii) Mgao wa mishororo

d) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama4)**

e) Bainisha toni ya shairi hili. **(alama1)**

f) Eleza mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa kwanza. **(alama2)**

g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama4)**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini
Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwa tayari kupanda na kushuka."

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka

Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijiokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla

**Maswali**

a) Fafanua mambo manne yanayokatisha tamaa katika shairi hili. **(alama4)**
b) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. **(alama4)**
i) Tashihisi
ii) Usambamba
iii) Mbinu rejeshi
iv) Tanakuzi
c) Fafanua aina tatu za taswira zilizotumika shairini. **(alama3)**
d) Onyesha aina tatu za urudiaji zinazojitokeza katika shairi hili. **(alama3)**
e) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. **(alama2)**
f) Tambua mifano miwili ya mistari mishata iliyotumika shairini. **(alama2)**
g) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. **(alama2)**

**8. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZE**

Mimi ni morani!
Nguli aliyekamilika
Nishatoka kumrarua simba dume
Kwa hii mikono miwili
Mimi ni shujaa asiyekanyaga kwa woga
Wala kubabaika
Simba mwenyewe ameungama
Mkuki wangu ni shahidi

Mimi ni jabali mtetemesha ardhi!
Azma yangu hairudi nyuma
Nguvu zangu hazimithiliki
Sina mzaha wala dhihaka
Mimi ni jasiri!
Ngao ndio hii hapa mkononi ni fumo nilirithi
Kujikinga na kulinda hadhi yangu
Yu wapi mwingine shujaa?

**Maswali**

a(i)Andika aina ya sifo hii. **(alama1)**

ii) Toa sababu nne kuthibitisha jibu lako la (i) hapo juu. **(alama4)**

iii)Tambua mbinu tano za lugha zilizotumiwa katika utungo huu. **(alama5)**

iv)Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii nyingi. Fafanua kwa hoja tano sababu za hali hii. **(alama5)**

v) Kwa kutumia hoja tano, eleza njia zinazotumiwa na jamii ya kisasa kuendeleza kipera hiki. **(alama5)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 5

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

1. *Andika Insha Mbili. Insha Ya Kwanza Ni Lazima.*
2. *Kisha Chagua Insha Nyingine Moja Kati Ya Hizo Tatu Zilizobaki.*
3. *Kila Insha Isipungue Maneno Mia Nne. 400*
4. *Kila Insha Ina Alama Ishirini. 20*
5. *Kila Insha Lazima Iandikwe Kwa Lugha Ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

**SWALI LA LAZIMA**

1. Wewe ni mtafiti wa maswala ya usalama nchini. Mwandikie barua Waziri wa Usalama wa Ndani barua ukimweleza sababu za wanafunzi wa shule za upili kujiunga na makundi ya wanamgambo, almaarufu Al Shabab.

**CHAGUA MOJA:**

2. Utandawazi una athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.
3. Andika insha inayodhihirisha maana ya 'Umdhaniye ndiye siye'
4. Kamilisha insha yako kwa maneno:

**...**sitaisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka kama nilivyoaibika siku hiyo.

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 5

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………….**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

***(a)*** *Andika jina lako na namba yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***(b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***(c)*** *Jibu maswali **yote.***
***(d)*** *Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***(e)*** *Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***(f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE: -**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**1. UFAHAMU (Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Ustawi wa dola lolote lile hutegemea mseto wa nguvu, maarifa chipukizi, uchapuchapu wa barubaru, pamoja na maarifa, upevu, uvumilivu na tajriba ya wazee. Tunaweza kuumithilisha ufanisi wa nchi na jumba la ghorofa lililojengwa juu ya tegemezo: msingi huu ukiwa imara, ghorofa nyingi zaweza kuinuliwa. Nayo imara ya tegemezo hutegemea vyuma imara visivyotetereka na vifaa vinginevyo. Zaidi ya haya yote, mafundi wahusika kama vile wasanifu mjengo, wahandisi, mafundi bomba na wengineo sharti wawe na ujuzi tosha ili kufanikisha kazi inayohusika. Katika taswira hii, twaweza kuelewa ni kwa nini baadhi ya nchi zimestawi huku nyingine zikiitwa ulimwengu wa tatu. Shida za nchi hizo ni kutozistawisha taaluma ambazo ndizo msingi wa maendeleo, hivyo huwa na walakini katika utekelezaji. Matokeo yake ni kulimatia.

Nchi nyingi humu barani mwetu zimekosa kustawi kutokana na kasoro nyingi tulizo nazo katika uimarishaji wa taaluma zetu. Sababu kuu ni kuwa, wengi wetu hukimbilia kutekeleza kazi mbalimbali hata bila ujuzi wowote kwa kazi hizo. Tabia kama hii inatokana na ukweli kuwa sisi hatujali kama tuna vipawa vya kufanya kazi fulani. Wengine huvunjwa moyo na waliowazingira kuwa vipawa vyao havifai. Hivyo, si ajabu kuona kijana aliye na kipawa fulani akikosa kukivuvia kwa sababu labda hata hatambui kuwa anacho.

Wengi wa wakembe wetu hukosa kuvitambua vipawa vyao, hivyo kukosa kuendeleza utaalamu unaohusiana navyo kwa kukosekana kwa **mtalaa** wa kuvichochea katika mfumo wa elimu. Mfumo wa elimu nchini Kenya kwa sasa unasisitiza wanafunzi kupita mtihani ili kuingia vyuoni. Hata hivyo, ni muhimu kuvikuza vipawa walivyo navyo vijana ili wavitumie katika siku za halafu. Vitambuliwe mapema shuleni bali si vyuoni. Kunao wanagenzi wengine ambao, licha ya kuvitambua vipawa vyao hawavifukutii kamwe, huvipuuza na kujisukuma katika taaluma ambazo hazikuwafaa kamwe. Kunao wanagenzi wengine ambao hutamani na kuingilia taaluma fulani, si kwa kuzipenda, bali kwa kuwa wandani wao wazishiriki. Hawajui kuwa kibaya chako si kizuri cha mwenzio. **Huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa.** Kuna wengine ambao huziandama taaluma fulani kwa kushurutishwa na wazazi au wadhamini wao. Nao vijana hukosa ukakamavu wa kujiamulia na kukubali shingo upande maamuzi hayo. Hata hivyo, kuna wale ambao hujitosa katika taaluma hizo bila kushurutishwa ili wapate hadhi. Matokeo ni kuwa kijana huzifanya kazi hizo kwa chati wala si kwa dhati. Wengine hujipenyeza kwa taaluma fulani eti kwa kuwa wamekosa nyingine. Si ajabu basi kutokana na ukosefu wa ajira kumwona mtaalamu wa mifugo akiwa mwalimu, mwalimu akiwa dereva na tabibu akiwa mkulima hali zaraa haimudu.

Ili kupata suluhu katika jambo hili, sharti kila mmoja wetu ashiriki katika kuitambua, kuikuza, kuikomaza na kutumia taaluma ya kila kijana. Twaweza kuuiga mfano wa Wazungu wafanyavyo kwao. Wao hujitahidi kuvitambua vipawa vya watoto wangali wachanga hali ambayo huwasaidia kuzikuza taaluma zao baadaye. Naye kijana akishajua atakachofanya, afaa kufanya utafiti ili kufikia kina cha taaluma yake.

# MASWALI

**(a)** Eleza sababu za watu kujishughulisha na taaluma zisizo zao**.** **(alama 2)**

**(b)** Eleza kikwazo cha ustawi wa nchi zinazoendelea**.** **(alama 1)**

**(c)** Taja mambo manne yanayostawisha taifa**.** **(alama 4)**

**(d)** Taja mambo matano yanayokwamiza uendelezaji wa vipawa miongoni mwa vijana. **(alama 5)**

**(e)** Kuna tofauti gani kati ya Waafrika na Wazungu katika ukuzaji wa taaluma? **(alama 2)**

**(f)** Eleza maana ya 'Huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa'. **(alama 1)**

**(g)** Eleza maana ya vifungu vifuatavyo vilivyotumika katika ufahamu**.** **(alama 2)**

**(i)** kulimatia

**(ii)** mtalaa

**2. MUHTASARI** **(Alama 15)**

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavovyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inaghadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba kuwa magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani. Damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini; vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumuua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki za kikatiba za Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao zimedumishwa. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kuhusu kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako yameishia kunasa raia wengi wasio na makosa.Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii inaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

## MASWALI

**(a)** Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi (alama 7,1 utiririko) (maneno 60-70)

**Matayarisho:**
**Nakala safi**
**(b)** Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6, 1 utiririko)

**Matayarisho:**

**(c)** Nakala safi

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

**(a)** (i) Eleza jinsi kitamkwa /u/ kinavyozuiliwa **(alama 2)**

(ii) Andika tofauti moja kati ya sauti hizi. **(alama 1)**

/t/ na /d/

**(b)** Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo**.** **(alama 2)**

Mwanajamii yule alijibu maswali yote kwa makini.

**(c)** (i) Eleza maana ya vitenzi vishirikishi**.** **(alama 1)**

**(ii) Tunga** sentensi moja moja kuonyesha aina mbili za vitenzi vishirikishi. **(alama 2)**

**(d)** Yakinisha sentensi ifuatayo. **(alama 1)**

Mtoto hakufundishwa wala kupewa vitabu.

**(e)** (i) Eleza maana ya silabi**.** **(alama 1)**

(ii) Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili**.** **(alama 2)**

**(f)** Ainisha viambishi katika sentensi hii kimuundo na kidhamira**.** **(alama 3)**

Wataonana

(i) Kimuundo:

(ii) Kidhamira

**(g)** Tumia nomino yoyote katika ngeli ya KU-KU pamoja na kiashiria kisisitizi cha karibu kutunga sentensi**.** **(alama 1)**

**(h)** Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali **isiyodhihirika** **(alama 1)**

**(i)** Tunga sentensi mbili ili kubainisha maana za neno: Jinsi **(alama 2)**

**(j)** Huku ukitoa mifano, eleza matumizi mawili ya alama ya kinyota katika uakifishaji. **(alama 2)**

**(k)** Eleza miundo mitatu ya vishazi tegemezi na kuitolea mifano mwafaka katika sentensi.**(alama 3)**

**(l) (i) Eleza** maana ya shamirisho kipozi. **(alama1)**

**(ii)** Benta alimlimia mamake shamba kwa trekta. Anza kwa **yambiwa** **(alama1)**

**(m) (i)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.

S – KN (N/Wθ) + KT (Ts+T+RH+E**)** **(alama 2)**

**(ii)** Changanua kwa matawi sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Kile chake kipya kinanipendeza mno.

**(n) Eleza** matumizi yoyote mawili ya kiambishi KU na kuyatolea mfano mmoja mmoja wa sentensi. **(alama 2)**

**(o)**Tunga sentensi sahihi ukitumia kivumishi cha ki ya mfanano na kielezi cha namna kitumizi. **(alama 2)**

**(p)**Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha silabi moja kinachomaanisha kuogopa katika kauli ya kutendeka**.** **(alama 2)**

**(q)** Eleza maana ya:

**(i)** Papo kwa papo kamba hukata jiwe**.** **(alama 1)**

**(ii)** Ua langu la waridi limechanuka**.** **(alama 1)**

(r) (i) Tunasema baraza la wazee …………………cha kuni na ……………..…… ya nguo (**alama 1)**

(ii) Ajuza ni kwa mwanamke mzee na …………………ni kwa msichana mchanga ilhali shaibu ni kwa mwanamume mzee na ………………………ni kwa mvulana aliyebaleghe. **(alama 1)**

## 4. ISIMUJAMII (Alama10)

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Niaje wasee! Midterm ilibamba lakini ilkua fupi sana, tumerudi books, huu ni mwaka wa mwisho tujikaze jo. Msifikirie hizo hepi zetu ni reality, kuchill ni jambo la maana jo! ama niaje bro…hustle ni real, bidii ndio itatuokoa

**(a)** Tambua sajili inayohusishwa na kifungu hiki **(alama2)**

**(b)** Eleza sifa zozote **nne** za kimtindo zinazojitokeza katika kifungu hiki**.** **(alama 4)**

**(c)** Eleza sababu **nne** zinazosababisha matumizi ya lugha ya aina hii**.** **(alama 4)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 5

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

*1) Jibu maswali **Manne** pekee.*
*2) Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.*
*3) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
*4) Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**MBELE YA SAFARI**

**1.** Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

**2.** Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti ,dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

**3.** Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari,utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari , juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

**4.** Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahala 'mekuwa dhiki
Wagombanio kipato,utashi haukatiki
Nakutabakari

**5.** Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita , mlima haupandiki
Basi sote 'kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

**6.** Tukiwa migongo  wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi , kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi ,Kuteremsha miliki
Wakaitapia

**7.** Wakafikia makazi,ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

**8.** Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema , kwa umati halaiki
Imezima nia yote ,kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

**a)** Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili**.** **(al2)**
**b)** Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa**.** **(al 6)**
**c)** Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia : **(al 4)**
i.Mizani
ii. Vina
**d)** Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. **(al 4)**
**e)** Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita **(al 4)**
**f)** Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. **(ala 2)**

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**
**Timothy Arege**
**BEMBEA YA MAISHA**
**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** (a.) Soma dondoo lifuatalo kasha ujibu maswali.

**Sara :** Mimi ninashukuru kwa hawa alionipa mungu. Nikitaka zaidi nitakuwa mchache wa shukrani.(kimya) Dina nimesemwa sanana kutukanwa kwa sababu ya hawa wasichana wangu. Wewe unajua yote yaliyosemwa, hadharani na faraghani. Si makanisani, si magengeni. Leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao, ninaridhika moyoni. Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika. (Anatokwa na machozi)

Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha.

i.) Changanua maudhui katika dondoo hili **(ala 3)**
ii.) Bainisha toni katika dondoo hili **(ala 2)**
iii.) Tambua mbinu tatu za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. **(ala 3)**
(b.) Jadili jinsi suala la utu linavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea Ya Maisha**(ala 12).**

AU.

**3.** Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(ala 20)**

**SEHEMU YA C: RIWAYA**
C. MOMANYI: **NGUU ZA JADI**
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."
(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**
(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano. **(alama 5)**
(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaa na ubinafsi katika nchi ya Matuo. **(alama 11)**

**AU**

**5.** "Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa nguvu akajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe. Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunza waja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia pia hujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.

**a)** Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

**b)** Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuza Riwaya ya Nguu za Jadi **(alama 5)**

**c)** Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawa katika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi. **(alama 10)**

## SEHEMU YA D :HADITHI FUPI

## *MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE*

*Jibu swali la 6 au 7*

### WINNIE NYARURI OGENCHE: ''SABINA''

**1.** ''Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.''

**a)** Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika.** **(alama 6)**

**b)** Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. **(alama 4)**

**c)** Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. **(alama 10)**

### YUSSUF SHOKA HAMAD: ''*Mzimu wa Kipwerere*''

**7."…**Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama."

(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(Alama 4)**

(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(Alama 4)**

(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(Alama 2)**

(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. **(alama 10)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***Swali la nane***

**8. a**) Ulumbi ni nini**?** **(alama 2)**

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii**?.** **( alama 6)**

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. **(alama 6)**

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. **(alama 6)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 6

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

JINA……………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………

INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

1. *Andika Insha Mbili. Insha Ya Kwanza Ni Lazima.*
2. *Kisha Chagua Insha Nyingine Moja Kati Ya Hizo Tatu Zilizobaki.*
3. *Kila Insha Isipungue Maneno Mia Nne. 400*
4. *Kila Insha Ina Alama Ishirini. 20*
5. *Kila Insha Lazima Iandikwe Kwa Lugha Ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

## 1. INSHA YA LAZIMA

Wewe ni mkuu wa Polisi Idara ya Trafiki Wilaya ya Muembe Mmoja. Kutokana na visa vingi vya ajali barabarani, waandikie ilani madereva na wananchi katika Wilaya yako kuhusu kutozingatia sheria za trafiki. Ilani hii itokee katika gazeti la 'Sauti'.

**2.** Vijana wengi nchini hawana ajira. Jadili mbinu mbalimbali za kubuni nafasi za kazi nchini Kenya kwa vijana.

**3.** Mchuma janga hula na wakwao. Andika kisa kudhibitisha methali hii.

**4.** Andika Insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

Nilipowakumbuka wenzangu, macho yaliingia kiwi, machozi yakanilengalenga**…**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 6

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

***Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)***

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. *Andika jina lako, shule na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
2. *Andika tarehe ya mtihani na utie sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
3. *Jibu maswali yote.*
4. *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa baada ya kila swali katika kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | 80 | |

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Kila mmoja wetu anafahamu jukumu muhimu linalotekelezwa na mashirika yasiyo ya kiserikali almaarufu kama NGOs katika shughuli ya kuleta maendeleo muhimu humu nchini.

Ni dhahiri kuwa maendeleo mengi ambayo tunajivunia kama jamii - hasa katika sehemu za mashinani - yametekelezwa na mashirika haya ambayo hufadhiliwa na serikali na mashirika ya kigeni. Sio tu miradi ya kupambana na ugonjwa hatari wa Ukimwi, maji ya kunywa, kilimo, ufadhili wa kimasomo n.k, bali hata inayohusu uhifadhi wa mazingira.

Hata hivyo, uchunguzi unaonyesha kuwa ingawa mashirika haya yanajivunia kutekeleza mengi, maendeleo ni machache mno ikilinganishwa na kiasi cha pesa ambacho kimetolewa na wafadhili. Madai yaliyotolewa na wanaharakati wa kutetea haki za kibinadamu nchini majuma kadhaa yaliyopita kuwa **walaghai** wa kitaalamu wameingia sekta hii **kuwapora** wafadhili pesa zao yana ukweli fulani.

Kuna mbinu kadhaa ambazo zinatumiwa na mashirika laghai kuwapora wafadhili pesa zao. Mbinu ya kwanza ni kupitia uandishi wa mapendekezo ya miradi isiyokuwepo. Mengi ya mapendekezo hayo huandikwa kwa lugha ya mvuto kuwashawishi wafadhili watoe fedha zao. Kuna uwezekano umewahi kukutana na wasomi waliobobea katika taaluma ya kuandika mapendekezo ya miradi kwa malipo. Hao ndio wajuao mambo ya kujumuishwa kwenye mapendekezo ya miradi ili kuwateka wafadhili. Kile wafanyacho ni kuandika mapendekezo na baadaye hupewa sehemu yao ya pesa hizo punde zinapotolewa.

Njia ya pili sio wizi wa wazi kwani huhusisha matumizi ya pesa kwa njia ambazo hazikukusudiwa. Badala ya kutumia pesa za wafadhili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopendekezwa, baadhi ya wasimamizi wa mashirika haya huweka pesa mifukoni mwao.

Viongozi wa mashirika mengine hutumia ufadhili huo kuzuru mataifa ya kigeni kwa kisingizio cha kuhudhuria makongamano ya maendeleo. Baadhi yao huwa hawaendi mbali; wao huandaa makongamano ya kukata na shoka kila mwezi katika hoteli kubwa kubwa nchini. Kinaya kilioje kuwa pesa zilizotafutwa kusaidia wajane katika vijiji vya mashambani zinatekeleza miradi bandia mijini? Inasemekana miradi ya baadhi ya mashirika hutekelezwa kimaandishi tu na maafisa wanaosimamia mashirika haya bila kuwahusisha waliolengwa.

Isitoshe, baadhi ya mashirika haya hutumia nyingi ya pesa zake kwa masulala ya utawala na usimamizi badala ya miradi ya maendeleo

**Maswali**

**a)** Taja jukumu muhimu linalotekelezwa na mashirika yasiyo ya kiserikali. **(alama 2)**

**b)** Ni miradi ipi ambayo imetekelezwa na mashirika haya? **(alama 5)**

**c)** Ni kwa nini maendeleo ambayo yametekelezwa na mashirika haya ni machache? **(alama 2)**

**d)** Ni mbinu zipi zinazotumiwa na mashirika laghai kuwapora wafadhili pesa zao? **(alama 4)**

**e)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kifunguni. **(alama 2)**

i) walaghai
ii) kuwapora

## 2. MUHTASARI (ALAMA 15)

Mfumo wa elimu wa 8.4.4 ulipoanzishwa nchini mnamo 1983, lengo kuu lilikuwa ni kuwapa wanafunzi maarifa ya kielimu hasa ya kiutendakazi ili kuwawezesha kijitegemea baada ya kumaliza masomo. Hata hivyo, wakosoaji wa mfumo huu wanasema kwamba yaliyomo kwenye mtaala ni mengi mno na kwamba mtaala wenyewe ni mzigo mzito kwa wanafunzi kando na kuegemea mno mitihani.

Hata baada ya kupunguzwa kwa idadi ya masomo ya kutahiniwa kwenye mfumo huu, mambo yalikuwa changamano zaidi wakati serikali ya NARC ilipoingia mamlakani na kuanzisha mfumo wa elimu ya msingi bila malipo mnamo 2003. Hatua hiyo ilisababisha idadi ya wanafunzi waliojiunga na shule za msingi kuongezeka maradufu-kutoka wanafunzi milioni 5 hadi wanafunzi milioni 8 mnamo 2009.

Licha ya kwamba mfumo wa elimu ya msingi bila malipo umesifiwa hapa na pale, wadadisi wa mambo hata hivyo wanatilia shaka masuala fulani kuuhusu. Mojawapo ya masuala haya ni viwango vya ubora wa elimu wanayopata watoto wetu. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na taasisi ya Uwezo Kenya mnamo Oktoba mwaka 2009, ilibainika kwamba mwanafunzi mmoja kati ya wanafunzi wanne katika kiwango cha shule ya msingi hufika katika darasa la tano bila ya kuwa na uwezo wa kujibu maswali ya masomo ya mwanafunzi wa darasa la pili.

Pamoja na hayo, uchunguzi huo ulibainisha kwamba takriban asilimia nne ya wanafunzi chini ya mfumo wa elimu ya msingi bila malipo husoma na kukamilisha masomo ya darasa la nane bila kupata maarifa ya kimsingi ya kusoma na kuandika au hata ujuzi wa kufanya hisabati za kimsingi

Hatua ambazo zimekwisha kuchukuliwa na serikali mpaka sasa-hasa ujenzi wa madarasa na amara ya kukidhi mahitaji ya idadi kubwa ya wanafunzi katika mfumo wetu wa elimu-hazijafanikiwa sana.

Aidha, ingawa serikali imeamua kuwaajiri walimu kwa mpango wa kandarasi, ili kukidhi nakisi ya takriban walimu 60,000 katika shule za msingi na upili, hatua hizo bado hazijatatua lolote!

Hali hii imesababisha uwiano kati ya mwalimu na wanafunzi kuwa 1:80 katika baadhi ya sehemu nchini na kufanya walimu kushindwa kutoa huduma bora kwa kila mwanafunzi. Katika hali ya kawaida, mwalimu mmoja anapaswa kuwafundisha wanafunzi kati ya 35 hadi 40. Hii inamaanisha kwamba mwalimu mmoja hushughulika idadi maradufu ya kiwango kilichoidhinishwa kote ulimwenguni. Katika mazingira kama haya, inakuwa vigumu mno kwa mwalimu kufundisha na kuwaridhisha wanafunzi-hasa wale ambao si wepesi wa kushika mambo.

Kuhusiana na vifaa vya kufundishia, bado kuna mushkili hasa ikichukuliwa kwamba kashfa iliyowakumba Waziri wa Elimu, Prof. Sam Ongeri, na aliyekuwa katibu katika wizara hiyo, Prof. Karega Mutahi, haikusuluhishwa. Kwenye kashfa hiyo, fedha zilizonuiwa kununua vifaa kama vile vitabu au kugharimia mpango wa elimu bila malipo zilitoweka kwa njia ya ajabu sana.

Hivi sasa, serikali imekaa tutwe huku watoto wetu wakiumia shuleni kana kwamba hakuna lolote lililotendeka. Shule nyingi hasa za msingi zina maktaba zilizojaa vitabu vya kiada. Hali hii bila shaka haiwachochei wanafunzi kuwa na msukumo wa kusoma kwa lengo la kujua mambo, husoma ili kupita mitihani tu. Utamaduni wa kusoma nchini unatiliwa shaka sana na hatujui ni lini utakapoimarika.

Watoto wanapaswa kukuzwa katika mazingira ya mfumo wa elimu unaothamini kusoma kwa minajili ya kupata maarifa na kupanua mtazamo wao, kinyume na sasa ambapo wanafunzi wanaotia fora katika mitihani hawajui chochote nje ya mitihani hiyo.

Tangu 2001, wadau katika sekta ya uandaaji na uchapishaji wa vitabu nchini Kenya, Uganda na Tanzania chini ya mwavuli wa Mradi wa Ustawishaji wa Vitabu Afrika ya Mashariki wamekuwa wakifanya juhudi za kimakusudi za kukuza na kupalilia utamaduni wa kusoma.

Nina wasiwasi kwamba kutokana na mlipuko wa 'teknohama' kote ulimwenguni, huenda watoto wetu wakaweka vitabu pembezoni na kushabikia mtandao wa intaneti na runinga badala ya kuchangamkia vitabu, majarida, magazeti na maandishi mengine kwenye karatasi.

## Maswali

**a)** Eleza kasoro za mfumo wa 8.4.4 kulingana na kifungu. (Maneno 25) **(alama 4)**

**Matayarisho**

**Jibu**

**b)** Mfumo huu wa elimu ya msingi bila malipo unatiliwa shaka kwa sababu ya mambo kadhaa. Fafanua. **(Maneno 75) (Alama 11, 2 za mtiririko)**

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**a)** Ukirejelea mkondo wa hewa kutoka mapafuni, eleza sifa za kimatamshi za ving'ong'o. **(alama 2)**

**b)** Kwa kuzingatia sehemu zilizopigiwa mstari, toa dhana inayojitokeza katika sentensi hii. **(alama 2)**

Alisugua meno, a<u>ka</u>oga a<u>ka</u>la kisha a<u>ka</u>ondoka.

**c)** Tumia neno vile kama **(alama 3)**

Kivumishi

Kiwakilishi

Kielezi

**d)** Yakinisha sentensi hii. **(alama 1)**

Kanisani simo wapatikanapo wezi.

i) Andika sentensi hii katika kinyume. **(alama 1)**

Mvua iliponyesha baba alienda kondeni.

ii) Andika hali ya ukubwa wingi. **(alama 2)**

Nyoka yule alimuuma mtoto mkono.

**e)** Tunga sentensi moja kudhihirisha kihusishi cha 'na' ya mtenda. **(alama 2)**

**f)** Onyesha dhana mbili zinazojitokeza baada ya kitenzi kunyambuliwa katika <u>kauli ya kutendeka</u>. **(alama 2)**

**g)** Eleza matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari. **(alama 2)**
Amke<u>ni</u> mwende duka<u>ni</u>!

**h)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. **(alama 2)**
Kasisi alitushauri, "Yafaa tamaduni ambazo hazitufai ziachwe".

**i)** Tumia kitenzi 'alikuwa' katika sentensi kama
i) Kitenzi kisaidizi. **(alama 1)**
ii) Kitenzi kishirikishi kikamilifu. **(alama 1)**

**j)** Tofautisha sentensi hizi. **(alama 2)**
i) Ningalimwona jana ningalifurahi
ii) Ningemuona jana ningefurahi

**k)** Kwa kuzingatia sehemu iliyopigwa mstari, toa maana inayojitokeza.
i) Wao <u>huenda</u> msikitini kila ijumaa **(alama 1)**
ii) Watoto <u>wacheza</u> majini. **(alama 1)**

**l)** Tambua chagizo katika sentensi hii. **(alama 1)**
Yeye huchapwa na mkewe mara kwa mara.

**m)** Weka shadda katika maneno haya. **(alama 1)**
i) Mtoto
ii) Mto

**n)** Huku ukitoa mfano eleza maana ya
i) Silabi wazi **(alama 1)**
ii) Silabi funge **(alama 1)**

**o)** Nyambua vitenzi hivi katika kauli ya kufanyiza.
i) Jua **(alama 1)**
ii) Kana **(alama 1)**

**p)** Onyesha viambishi katika sentensi hii. **(alama 3)**
Nitamtafutisha

**q)** Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya maneno haya
i) Figo **(alama 1)**
ii) Pigo **(alama 1)**

**r)** Pambanua sentensi hii ukitumia kielelezo matawi.
Japo alifanya kazi zote hakulipwa. **(alama 3)**

**s)** Tunga sentensi ukitumia 'O' rejeshi ya tamati. **(alama 1)**

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**a)** Eleza mitazamo miwili kuhusu chimbuko la lugha ya kiswahili nchini Kenya. **(alama 2)**
**b)** Eleza mambo manne yaliyochangia kuenea kwa lugha ya kiswahili zama za ukoloni. **(ala 8)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 6

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA…………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

*a)* *Jibu maswali* ***Manne*** *pekee.*
*b)* *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***Lazima****.*
*c)* *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
*d)* *Usijibu maswali* ***Mawili*** *kutoka* ***Sehemu moja****.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU A:**

**FASIHI SIMULIZI**

**1. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwana mbee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na mito
Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti
Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso wa radi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika
Kuona kifua changu cha manyoya ya kanga wakatetemeka
Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama wakakimbia
Mkuki wangu ulipaa kama umeme
Wote wakalala
Mifugo wakanifuata…
Mko wapi vijana
Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

**Maswali**

a) Tambua kipera ulichokisoma na udhibitishe jibu lako **(al. 2)**
b) Tambua sifa za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu **(al. 2)**
c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vine vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsineni **al. 4)**
d) Fafanua sifa nne za kipera hiki **(al. 4)**
e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. **(al. 4)**
f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia **(al. 4)**

## SEHEMU YA B: USHAIRI

**Jibu swali la 2 au 3**

2. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wao ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurai Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanunua mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza vunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Ninacho change killo, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadi ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. **(alama 1)**

b) Fafanua mambo **matatu** ambayo nafsineni analalamikia. **(alama 3)**

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(alama 3)**

(i) Idadi ya vipande katika kila mshororo

(ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti

(iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

d) Andika ubeti **wa nne** katika lugha nathari. **(alama 4)**

e) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. **(alama 2)**

g) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

h) Fafanua muundo wa ubeti **wa tano**. **(alama 3)**

**3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tilichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisa kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hiii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa.
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha **(al. 2)**
b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili **(al. 2)**
c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume **(al. 2)**
d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili **(al. 4)**
e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili **(al. 2)**
f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi **(al. 4)**
g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? **(al. 4)**
   i) Mbari
   ii) Msununu
   iii) Ngariba
   iv) Uvundo

**SEHEMU C: TAMTHILIA; BEMBEA YA MAISHA – TIMOTHY M. AREGE**

**Jibu Swali la 4 au 5.**

4. **"Huku ndiko kuvumilia hasa. Tazama faraja ilivyoalika sasa"**

a) Weka dondoo hili katika muktadha. **(alama 4)**
b) Eleza sifa za msemaji katika dondoo. **(alama 6)**
c) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

**AU**

**5.**

**(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho.** **(alama 10)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandiwala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe)*. Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

b) Bainisha toni ya dondoo hili. **(alama 2)**

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima**.(alama 8)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**Jibu swali la 6 au 7**

**6. Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua***

"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake **(al. 4)**

(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii **(al. 6)**

(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii **(al. 10)**

**7. D.W .LUTOMIA : *Msiba wa kujitakia***

**Wetu ni wetu ,hata akiwa mbaya …ni wetu.hatuna budi kuchagua yeye .lisilobudi hubidi.**

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4)**

(b)Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hii. (**alama 4**)

(c)Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.jadili.(**alama 12**)

## SEHEMU YA E: RIWAYA- NGUU ZA JADI

**8.** Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa samba. <u>Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi.</u> Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasisi hao?.

(a) Eleza mbinu nne za mimtindozinazojitokeza katika dondoo **(al 4)**

(b) Eleza sababu za msemaji kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari **(al 10)**

(c) Eleza umuhimu wa msemaji katika kujenga ploti ya riwaya hii **(al 6)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 7

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA………………………………………………………………………………….**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

1. *Andika Insha Mbili. Insha Ya Kwanza Ni Lazima.*
2. *Kisha Chagua Insha Nyingine Moja Kati Ya Hizo Tatu Zilizobaki.*
3. *Kila Insha Isipungue Maneno Mia Nne. 400*
4. *Kila Insha Ina Alama Ishirini. 20*
5. *Kila Insha Lazima Iandikwe Kwa Lugha Ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

**1. Lazima.**

Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji wa vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi. **(Alama 20)**

**2.** Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili. **(Alama 20)**

**3.** Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa. **(Alama 20)**

**4.** Andika insha itakayomalizikia kwa;

**…**walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia. **(Alama 20)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 7

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

JINA…………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………

INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

*(a)Andika jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(b)Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

*(c) Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

## 1.UFAHAMU (alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa

kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

**MASWALI**

**(a)** Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. **(alama 1)**

**(b)** Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. **(alama 1)**

**(c)** Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. **(alama 2)**

**(d)** Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo**.** **(alama 2)**

**(e)** Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. **(alama2)**

**(f)** Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? **(alama2)**

**(g)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(alama 3)**

**(h)** (i) inasigana..........................................................................................................

(ii)yameghoshi……………………………………………………………………………………

(iii)vighairi……………………………………………………………………………………

**2 UFUPISHO (alama 15)**

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa

yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

**(a)** Fupisha aya ya pilina tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**(b)** Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.
(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**3.MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

**(a)** Taja vipasuo sighuna **(alama 2)**

**(b)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:
kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi **(alama 2)**

**(c )** Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi **(alama 2)**
Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .

**(d)** Sahihisha
Mwalimu mwenye alikuja jusi anafudisha Kiswahili vizuli. **(alama 2 )**

**(e)** Yakinisha sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Hakuwapiga wala kuwalaghai.

**(f)** Eleza viambishi katika neno lifuatalo **(alama 3)**
Walichokilalia

**(g)** Bainisha vivumishi vilivyo katika sentensi ifuatayo**:** **(alama 2)**
Wanafunza wote wenye nidhamu watapewa tuzo kubwa na mwalimu wao.

**(h)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 4)**
Yohana na Otieno hucheza kandanda.

**(i)**Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano. **(alama 3)**

**(j)**Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. **(alama 2)**
Askari jela alimwuliza Kendi kama alidhani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja.

(k) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. **(alama 1)**
IK+KI+KI+KI

**(l)** Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo**.** **(alama 2)**
**(i)** kibainishi
**(ii)**parandesi

**(m)** Tumia neno –baya kama**:** **(alama 2)**
(**i)** kiwakilishi
**(ii)**kielezi

**(n)** Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya tendewa. **(alama 2)**

**(o)**Badilisha maneno yaliyopigiwa mstari yawe vitenzi. **(alama 2)**
Yunis amepata faida kutokana na ukulima.

**(p)Kwa** kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: **(alama2)**
Tinga amewafanya ng'ombe wake wanywe maji.
(Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie 'amewafanya')

**(q)**Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-U. **(alama 2 )**

**(r)** Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. **(alama 2)**
Umu alimwandikisha mkewe.

**(s)**Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika. **(alama 1)**

## 4.ISIMU JAMII (Alama 10)

**(a) Lahaja** huainishwa katika makundi mawili. Yataje **(alama 2)**

**(b)** Eleza sifa zozote nne za lugha ya taifa. **(alama 4)**

**(c)**Tolea ushahidi namna nne kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa. **(alama 4)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 7

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

JINA……………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………

INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

- *Jibu maswali manne pekee. Swali la kwanza ni la lazima*
- *Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU YA A ;**

## SWALI LA LAZIMA-FASIHI SIMULIZI

**1.**

**a)** Fafanua maana ya lakabu **(alama 2)**

**b)** Sifa za lakabu ni zipi **(alama 5)**

**c)** Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii? **(alama 3)**

**d)** Jadili manufaa ya utafiti katika fasihi simulizi. **(alama 10)**

## SEHEMU YA B:TAMTHILIA

## BEMBEA YA MAISHA (TIMOTHY M. AREGE)

### Jibu swali la 2 au 3

**2.. ‘’** Lakini ndiyo tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama...kama…kama vile tambara bovu.’’

a. i)Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. **(Alama 4 )**

ii)Tambua mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo. **(Alama 2)**

b) Fafanua **umuhimu wa msemaji** katika kujenga ploti. **(Alama 4)**

c) **Utamanduni** huthaminiwa sana na jamii ya tamthilia ya Bembea ya Maisha. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano **kumi** mwafaka tamthiliani. **(alama 10)**

**3.** Beni:Afadhali hao.Mjukuu wangu hatofautishi kondoo,mbuzi na mbwa.Wote hao kwake yeye ni mbwa!(*wanacheka wote)*

Yona: Inachekesha.

***Swali***

Mazungumzo haya kati ya Beni na Yona yanabainisha tofauti iliopo kati ya suala la *usasa na ukale*. Kwa kutoa mifano **kumi** inayoonyesha usasa na **kumi** inayoonyesha ukale,linganua masuala haya. **(alama 20)**

## SEHEMU C: RIWAYA

## Clara Momanyi: Nguu za Jadi

### Jibu swali la 4 au 5

**4.** “Tangu lini mke amuulize mumewe kule aendako au atokako?.....Ama kweli, wanawake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee.”

i) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. **(alama4)**

ii) Kwa kutoa mfano,**taja mbinu ya lugha** iliyotumika**.** **(alama2)**

iii) Eleza **umuhimu wa** msemaji **(alama4)**

(iv) Kwa kutoa mifano **kumi** kutoka riwayani, fafanua jinsi **mwanamke amesawiriwa** katika jamii ya Matuo. **(alama 10)**

**5. Jamii** ya Matuo katika riwaya ya ‘Nguu za Jadi’ imekumbwa na **usaliti** si haba. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani, onyesha ukweli wa kauli hii. **(alama20)**

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

D.W Lutomia na Phibbian Muthama: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine* **Jibu swali la 4 au la 5**

**6.“**Enhee! Mpaka sasa hukupata nafasi ya kupiga simu, au angalau kutuma arafa?” “Samahani ... ulipopiga nilikuwa barabarani, singeweza kupokea simu.”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 5)**

(b) Tambua toni katika dondoo hili. **(alama 1)**

(c) Eleza vipengele viwili vya kimtindo katika dondoo hili. **(alama 2)**

(d) Eleza sifa nne za aliyekuwa barabarani akapigiwa simu na kushindwa kuipokea. **(alama 4)**

(e) Harubu ni sehemu ya maisha ya binadamu. Hakiki kauli hii kwa hoja nane kwa kurejelea hadithi Harubu ya Maisha. **(alama 8)**

**AU**

**7…**akikiomba radhi kile kitawi cha mti kilichonasa kwenye kazu yake ya rangi ya udongo iliyoficha kiwingu cha nongo kwa kukosa kuoshwa tangu ainunue! Nikauacha mpambano ule kati ya mzimu na mwenye dhamana ya mzimu ambao sina shaka ulidumu hadi asubuhi pale wanakijiji walipofika kushuhudia siri nzito iliyomezwa na mzimu ule waliokuwa wakiogopa na kuamini kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka!

(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

(b) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo. **(alama 4)**

**g)** Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha ‘mwenye dhamana ya mizimu’ na wenzake kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini Mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka. **(alama 8)**

## SEHEMU E: USHAIRI

**8. (Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata)**

**RABI HUMLIPIZIA**

Pungueni uonezi, wanyonge kuwaonea
Kuwafanya wao mbuzi, mazizini kuwatia.
Muogopeni Mwenyezi, haki mkiwapatia.
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Rabi kumeza hawezi, dhuluma isiyo njia,
Atatoa uamuzi, haki inayopotea,
Daima kwake machozi, kuna kilio kulia,
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Niyanenayo sadiki, alikilini kuyatia,
Aloshikilia haki, hatafikwa na hatia,
Punguzeni unafiki, kuzua mkichelea
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Haki haifichamiki, japo iwe myaka mia,
Mwenyezi Mungu mwehaki, haki ataifichua
Awatenge wanafiki, haki mnaoumbua,
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Kuna kundi lake laki, limekaa langojea,
Kukalia unafiki, mwashibota kuwania,
Punguzeni mwabonaki, mumde mola jalia
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Rabi atawafedhehi, haki wanayoumbuwa,
Na mwisho awakebehi, avunje wenu uluwa,
Mwenzi wenu nimewahi, Mungu ameniokowa,
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

***(kutoka: Diwani ya Akilimali, Akilimali, S.E.AL.B; Uk 54)***

**<u>Maswali</u>**

**a)** Taja umuhimu ya kutenda haki. **(alama 4)**
**b)** Taja mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili. **(alama 2)**
**c)** Shairi hili linaweza kuwa katika bahari mbili. Zitaje **(alama 2)**
**d)** Taja na ueleze mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi uliotumika. **(alama 2)**
**e)** Mshairi alikuwa na dhamira ipi alipotunga shairi ili. **(alama 2)**
**f)** Andika ubeti wa 3 kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**
**g)** Eleza muundo wa ubeti 2 **(alama 2)**
**h)** Fafanua maana ya :
(i) Awatenge wanafiki, haki mnaoumbua. **(alama 2)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 8

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………………  SAHIHI…………………………**

**INDEX NO…………………………………………  NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

1. *Andika Insha Mbili. Insha Ya Kwanza Ni Lazima.*
2. *Kisha Chagua Insha Nyingine Moja Kati Ya Hizo Tatu Zilizobaki.*
3. *Kila Insha Isipungue Maneno Mia Nne. 400*
4. *Kila Insha Ina Alama Ishirini. 20*
5. *Kila Insha Lazima Iandikwe Kwa Lugha Ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

# MASWALI

**1. Lazima**

Kumekuwa na visa vingi vya utovu wa nidhamu shuleni mwenu. Ukiwa katibu wa viranja, andika kumbukumbu za mkutano uliojadili vyanzo vya utovu huo na suluhisho lake.

**2.** Usafiri wa pikipiki za bodaboda una manufaa zaidi kuliko hasara. Jadili.

**3**. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.

**4**. Tunga kisa kitakachomalizia maneno yafuatayo:

**…**nikamtazama Marina huku machozi yakinitiririka njia mbilimbili kutokana na majuto yaliyonijaa.

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 8

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

***Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)***

## MAAGIZO

*a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*c) Jibu maswali **yote.***
*d) Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**1. UFAHAMU: ( Alama 15)**

Meli alipokivuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya Tungambele alikuwa na azma ya kusoma kwa bidii ili kuinukia kuwa kijana wa kutegemewa na jamii yake. Alikuwa kalelewa katika familia yenye pato wastani. Akasoma kwa juhudi za wazazi wake hadi darasa la nane alipokwangura alama za kumwezesha kujiunga na shule hii ya kifahari. Meli alijua kwamba alikuwa mwanagenzi, si katika masomo ya shule ya upili tu, bali pia katika maisha ya jijini ambamo shule hii ilipatikana. Kwa kweli hii ndiyo ilikuwa mara yake ya kwanza kutia guu kwenye jiji hili ambalo habari zake akizisoma, ama katika magazeti machache yaliyowahi kufika kijijini, au kupitia somo la Elimujamii. Hata hivyo, Meli hakuwa mtu wa kuogopa au kunywea machoni mwa changamoto. Alijiambia kwamba kwa vyovyote vile atapambana na maisha haya mapya.

Saa mbili kamili asubuhi ilimpata Meli kapiga foleni katika afisi ya kuwasajili wanafunzi wageni. Wasiwasi wa aina fulani ulianza kumnyemelea alipotazama hapa na pale bila kuona dalili ya mja yeyote aliyemfahamu. Alijihisi kama yule kuku mgeni ambaye mwalimu wake alishinda kuwaambia kuwa hakosi kamba mguuni. Hata hivyo aliupiga moyo wake konde na kujiambia kuwa kuja kwake hapa kulitokana na juhudi zake mwenyewe na katu hatauruhusu ugeni wa mazingira kuifisha ari yake ya masomo.

Usajili ulikamilika, naye Meli na wenzake wakajitosa katika ushindani wa kimasomo jinsi waogeleaji wajitumbukizapo kidimbwini wakapiga mbizi, baadhi wakiambulia ushindi na wengine wakifedheheka kwa kushindwa. Meli na wenzake walibainikiwa kwamba wote walikuwa mabingwa kutoka majimbo na wilaya zao. Ilimbidi kila mmoja wao kujikakamua zaidi ili kuelea katika bahari hii ya ushindani. Muhula wa kwanza ulishuhudia kishindo cha Meli kubwagwa chini na majabali wenzake. Alijipata miongoni mwa wanafunzi kumi wa mwisho; au kama alivyozoea **kuwatania** wenzake katika shule ya msingi, "wanafunzi kumi bora kuanzia mwisho"! Hili lilimwatua moyo Meli na kumfanya kutahayari. Alifika kwao amejiinamia kama kondoo aliyeumia malishoni. Akawataka wazazi wake wambadilishie shule lakini wakakataa.

Muhula wa pili na wa tatu mambo yalikuwa yaleyale. Meli akahisi kama askarijeshi aliyeshindwa kabisa kutambua mbinu za kuwavizia maadui. Akaona kwamba njia ya pekee ni kujiunga na wenzake kama yeye katika vitendo vya utundu kama vile kuvuruga masomo kwa kupiga kelele darasani, kupiga soga bwenini na hata kuvuta sigara. Mwanzoni alichukia vitendo hivi lakini alimeza mrututu akisema kwamba ndiyo njia ya pekee ya **kujipurukusha**na aibu. Wazazi wa Meli hawakusita kutambua mabadiliko katika hulka ya mwanao. Wakajaribu kumshika sikio nyumbani lakini akawa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Wakawahusisha wataalamu wa ushauri nasaha ambao waliwaambia kuwa Meli hakuwa na tatizo lolote la kuyadumu masomo. Kile alichokosa ni kujiamini tu.

Wazazi wa Meli waliona kuwa ni muhimu kuwahusisha walimu katika kutatua tatizo la mwanao. Mwanzo wa muhula wa pili uliwapata wazazi hawa afisini mwa naibu wa mwalimu mkuu. Mazungumzo kati ya wazazi, naibu wa mwalimu mkuu na mwalimu wa darasa la Meli yalidhihirisha kwamba walimu walikuwa wamemuasa Meli kuhusu kujiingiza katika makundi yasiyomfaidi lakini rai zao ziliingia katika masikio yaliyotiwa nta. Aliyopenda Zaidi Meli nishughuli zilizomtoa nje ya shule kama vile tamasha za mziki, ukariri wa mashairi na drama.

Mazungumzo yalibainisha kwamba Meli alihitaji ushauri na uelekezaji Zaidi kutoka kwa mtaalamu wa nasaha pale shuleni.

Meli alianza vikao na mtaalamu huyu ambaye pia alimpendekezea Meli ushauri zaidi kutoka kwa washauri marika. Hili lilimchangamsha zaidi Meli kwani aliwaona hawa kama wenzake waliojua changamoto zake. Juhudi za mtaalamu wa nasaha na washauri marika zilifua dafu. Mwisho wa kidato cha pili ulishuhudia mabadiliko makuu katika hulka na utendaji kimasomo wa Meli. Aliukata kabisa uhusiano wake na marafikiwaliompotosha na kuanza kuandamana na wanafunzi waliotia juhudi masomoni. Polepole alama zake ziliimarika. Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yalimweka kwenye safu ya wanafunzi bora zaidi nchini.

**a)** "Wanafunzi wawapo shuleni hukumbana na changamoto nyingi". Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hoja sita kutoka kwenye taarifa**. .** **(alama 6)**

**b)** Eleza mchango wa washikadau mbalimbali katika kumsaidia Meli kupata ufanisi masomoni.**(al 4**

**c)** Bainisha mbinu **tatu** za lugha ambazo msimulizi anatumia katika kuwasilisha ujumbe wake katika kifungu. **(alama 3)**

**d)** i. Andika kisawe cha '**kijipurukusha'** kwa mujibu wa taarifa **(alama 1)**

ii. Andika maana ya '**kuwatania'** kulingana na taarifa. **(alama 1)**

## 2. UFUPISHO (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Bei ghali ya vyakula ni jambo linalowaathiri wakenya wengi kwa hivi sasa. Inasikitisha kupata kwamba bei ya unga wa ugali imepanda hadi sh. 200. Ni wazi kwamba familia nyingi nchini hukosa lishe lao kutokana na kufumka kwa bei ya bidhaa muhimu. Hata hivyo ibainike kwamba nchi isiyowakimu raia wake kwa chakula ni sawa ng"ombe aliyeshindwa kumnyonyesha ndama wake.

Kwa muda mrefu, viongozi wamekuwa wakipambana na tatizo la ukosefu wa chakula. Msimu wa kiangazi unapobisha hodi, watu wengi hasa wale wahitaji hupukutika kutokana na mngato wa njaa. Japo serikali na wafadhili hutuma vyakula vya msaada kwa jamii zilizoathirika, chakula hiki huwa kama nguo ya kuazima, na bila shaka ya kuazima haikidhi haja.

Mojawapo ya vyanzo vikuu vya uhaba wa chakula ni kiwango cha chini cha uzalishaji na uhifadhi wa chakula chenyewe. Zipo seheu nyingi ambazo ni kame nchini.sehemu hizi hukabiliwa na ukosefu wa maji kwani, ama mvua hainyeshi au inaponyesha haitoshelezi mahitaji ya mimea. Mimea mingi hujikaukia ikiwa michanga na kudhihaki juhudi za wapanzi. Zipo sehemu katika nchi hii ambazo huenda kwa misimu hata mitano bila kupata zao lolote kutoka mashambani. Hali ikiwa hivi makali ya uhitaji huzidi na wakazi wa sehemu hizi hulazimika kuwa wategemezi kwa majirani na serikali. Wengine wanapokosa chakula kabisa huazimia kula visivyoliwa.Wanaamwa la mbwa baada ya kukosa la mama.

Hali kadhalika japo zipo sehemu zingine ambazo hazina tatizo la ukame, mbinu hasi za kilimo husababisha utoaji wa mavuno haba, hivyo kutojitosheleza kwa chakula. Bilas haka wanapopanda ovyo wanavuna ovyo. Kuna wakulima ambao hupalilia mmomonyoka wa udongo kwa kulima kando kando ya mito, kupanda zao lile lile katika sehemu ile ile ya ardhi miaka nenda miaka rudi, na kutopanda mimea ambayo hukinga tabaka la juu la udongo dhidi ya kumomonyolewa na maji au upepo. Matokeo ya haya yanaweza kutabiriwa; udongo wenye rutuba huoshwa na mashamba kutwaa utasa ambao huzidisha kuzalisha kwa chakula haba. Wakulima wengine hukaidi wito wa kupanda mimea ambayo hustahimili ukame kama vile mbaazi mihogo, mtama na wimbi. Baadhi

ya wakulima hufuga mifugo wengi ambao hushindwa kustahimili kiangazi. Si ajabu kupata kwamba katika baadhi ya maeneo mizoga ya ngombe na hata ngamia imezagaa kote tanuri la kiangazi linapofanya kazi yake.

Sehemu zingine zimebarikiwa na ukwasi wa chakula. Hata hivyo baadhi ya wakazi wa sehemu hizi hawana mwao kuhusu umuhimu wa lishe bora. Wapo wanaodhani kuwa chakula ni chakula bora tumbo lipate haki. Hawa hula vyakula kama vile viazi, mahindi, na wengine nyama bila kujua wanahiyaji vyakula vyenye virutubisho muhimu, yani wanga, protini , vitamini na madini. Wapo wanaodhani kuwa protini pekee ni nyama. Hawa hula nyama mawio na machweo, matokeo yakiwa kuambulia magonjwa kama vile shinikizo la damu.

Katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa chakula, serikali kupitia wizara husika imeanzisha miradi ya kuhakikisha kuwa kuna uzalishaji wa chakula kwa kiwango cha kuridhisha. Serikali ya Ruto sasa imepunguza bei ya mbolea hadi sh 3500 ili kuwawezesha wakulima kupanda chakula kwa wingi. Visima na mabwawa ya maji pia vitachimbwa katika maeneo kame ili kunyunyuzia mashamba maji. Baadhi ya wakulima wameanza kupanda mimea ambayo inapevuka na kutoa mazao kwa haraka ipo mimea ya kuatika ambayo hutoa matunda baada ya muda mfupi, hivyo kusaidia kupunguza makali ya njaa. Wafugaji wengine wameanzisha miradi ya kufuga kuku wa kututumuliwa. Hawa hukuwa na kukomaa kwa muda mfupi na huweza kutoa nyama na mayai. Wafugaji wa kuku hawa huweza kuwauza kununua aina nyingine ya chakula.

Wakulima pia wanahimizwa kutumia njia za kisasa za kuzalisha na kuhifadhi chakula.chakula kinapohifadhiwa vyema, hata mvua isiponyesha raia huweza kujitegemea. Ikiwa maghala ya halmashauri za kuhifadhi chakula nchini hayahifadhi chakula mara nyingi hulazimika kuagiza chakula kutoka nje kiangazi kinapojiri. Aidha chakula kisipohifadhiwa vyemahuishia kuharibika na kuhasiri wanaokila ikawa msiba juu ya mwingine.

Ni muhimu kufahamu kuwajukumu la kupambana na ukosefu wa chakula ni la kila raia. Hali ya kungojea kila mara kulishwa na serikali inatufanya kuwa wategemezi Zaidi. Wadogo wadogo ambao huuza vyakula kwa bei ya chini sana mara tu wanapovitoa mashambani wanapaswa kujiasa dhidi ya mazoea haya na kujua kuwa akiba haiozi. Wanaoishi katika sehemu za vinamasi wasaidiwe kuzitunza sehemu hizi na kuzitumia kwa njia endelevu. Vijana wahimizwe wawaunge wazee mkono kushughulikia kilimo katika sehemu za mashambani badala ya kuhamia mijini kutafuta kazi za ajira ambazo ni haba.

**a)** Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 100**.** **(alama 9, 1 ya mtiririko)**

**Matayarisho**

**Jibu**

**b)** Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, eleza njia sita za kukabiliana na uhaba wa chakula. (maneno 85) (alama 6, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3.MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**a)** Eleza maana ya kipashio kidogo cha lugha**.** **(alama 1)**

**b)** Andika maneno yenye sifa zifuatazo**:** **(alama 2)**

i) kikwaruzo ghuna cha ufizi, vokali ya chini-wastani, kizuiwa ghuna cha midomo, kiyeyusho cha midomo, irabu ya chini-kati

ii) Kipua ghuna cha ufizi, kipasuo cha ufizi, irabua ya mbele-juu, nazali ghuna ya midomo, irabu ya nyuma-juu.

**c)** Ainisha uamilifu wa kisarufi wa mofimu kwenye neno hili**.** **(alama 3)**

Lilimjisha

**d)** Tunga sentensi **moja** kuonyesha matumizi **mawili**ya **"tu"**. **(alama 2)**

**e)** Unda kitenzi kutokana na nomino **toba** kisha ukitungie sentensi**.** **(alama 2)**

**f)** Yakinisha kwa kutumia kiambishi cha masharti ya uwezekano kwa wingi**.** **(alama 2)**

Usiposoma kwa bidii hutofaidika.

**g) Tumia** nomino ya ngeli ya mahali dhahiri pamoja na kivumishi kirejeshi cha kati kwa sentensi. **(alama 2)**

**h)** Andika kinyume cha sentensi hii. **(alama 2)**

Mjomba alimtwika mwanawe mzigo akabana mlango.

i) Bainisha kijalizo katika sentensi ifuatayo**.** **(alama 1)**

Tajiri huyo shupavu ana magari makubwa mno.

*j) Tunga* sentensi kwa kutumia chagizo cha ulinganisho. **(alama 2)**

**k)** Andika upya sentensi kwa wakati uliopita hali endelevu, kauli ya tendesheka**.** **(alama 2)**

Wenyeji wamewapokea wageni kwa taadhima.

**l)** Tunga sentensi **moja** kuonyesha maana mbili za neno **tema.** **(alama 2)**

**m)** Ainisha aina ifuatayo ya sentensi kiutendakazi. **(alama 1)**

Safari imekuwa ikitusumbua sana.

**n)** Onyesha kiima na utambue muundo wake katika utungo huu. **(alama 2)**

Pesa zote zilihifadhiwa na mwekahazina shujaa.

**o) Tumia** kishazi tegemezi kwenye sentensi kuonyesha vigezo vifuatavyo**.** **(alama 2)**

i) Wakati

ii) Jinsi

**p)** Changanua kwa kielelezo cha mistari. **(alama 4)**

Aliponijia kwa mkopo, nilikuwa nasali sebuleni.

**q)** Andika upya kwa kuanza na yambwa tendwa**.** **(alama 2)**

Mvua iliwanyea wanunuzi sokoni hivi majuzi.

**r) Tunga** sentensi katika udogo ukitumia kihusishi cha uhusiano**.** **(alama 2)**

**s)** Eleza matumizi ya kiambishi **po** katika sentensi**.** **(alama 2)**

Achezapo anapofika sisi hushangilia.

**t) Twasema** oyee tunapofurahia jambo**………………………………..**tunapotahadharisha na **………………** Tunapotoa himizo **(alama 2)**

## 4: ISIMU JAMII **(alama 10)**

***Soma makala haya kisha ujibu maswali;***

Rafiki yako amezongwa na mambo magumu na anafikiria suluhu ni kujiua umepewa jukumu la kumshauri.Fafanua sifa **kumi** za lugha utakayotumia ili kufanikisha ujumbe wako.

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 8

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

*1) Jibu maswali **Manne** pekee.*
*2) Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.*
*3) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
*4) Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU A:FASIHI SIMULIZI** **(ALAMA 20)**

**1. LAZIMA**

Hamkuona jinsi tulivyowapiga mabao
Hamkuona vile tuliwachezea kama watoto,tuliwachenga kila mara
Hamkuona waliponea tundu la sindano tungewapiga mabao kumi na mbili
Ingekuwaje timu mbovu kama hii kucheza na miamba kama sisi?
Niliwafunga baada ya sekunde wakati ule nitashindwaje leo?

**Maswali**

a) i)Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanue. **(alama 2)**

ii) Fafanua sifa zozote sita za kipera ulichotambua katika (a) **(alama 6)**

b) i) Wewe ni miongoni mwa wale wanaotambiwa ngano katika kikao cha utambaji wa ngano.Fafanua mambo sita ambayo unaweza kuchangia ili kufanikisha uwasilishaji wa utambaji. **(alama 6)**

ii) Umeanza mikakati ya kukusanya data kupitia mbinu ya mahojiano. Eleza changamoto sita ambazo unaweza kukumbana nazo nyanjani. **(alama 6)**

**SEHEMU B:TAMTHILIA**

**Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha**

*Jibu swali swali la 2 au la*

**2**. Mama!Mamangu mzazi ni mboni ya jicho kwetu.Ananihitaji kipindi hiki cha lala salama.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Tambua mbinu tatu za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 3)**

c) Fafanua sifa za mhusika '***mamangu mzazi'*** ukirejerea tamthlia nzima. **(alama6)**

d)Fafanua majukumu ya elimu katika jamii kwa mujibu wa tamthlia ya Bembea ya Maisha. **(alama 7)**

***Au***

**3.** "Sara: Si neno mama!(kimya).Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi.Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha.Maisha yetu ni mfano wa mbegu iliyopandwa .Mbegu hiyo haina budi kuoza kwanza ndipo ioteshe mche upendezao."

a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 8)**

b) "Sasa hali ni tofauti. Tamaduni,mila na desturi zetu zimezidi kuyakubali mabadiliko."

i) Eleza nafasi ya msemaji wa kauli katika (b),katika kuendeleza tamthilia husika. **(alama 6)**

ii) Wahusika mbalimbali katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha* wamebuni mikakati mwafaka ili kujikomboa kutokana na kauli zilizopigiwa mstari.Fafanua mikakati **sita** kutoka tamthliani. **(alama 6)**

## SEHEMU C: RIWAYA

**Clara Momanyi: Nguu za Jadi**

**Jibu swali la 4 au 5**

**4.** Hakujua akimbilie wapi.Sasa afanye nini?Alilitupia lile jinyama lakini likahepa.Alihisi maisha yake yamo hatarini.

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(alama 4)**

b) Kwa kutoa mfano,tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili **(alama2)**

c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika riwaya hii. **(alama 6)**

d) Jamii ya nchi ya Matuo imesheheni vikwazo ambavyo vinakaa kama nguu,na kutoka jadi nguu hizi zimeathiri kwa upana usawa katika jamii.Tathmini kauli hii kwa hoja **sita.** **(alama 6)**

***au***

**5.** Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa simba. <u>Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi.</u> Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasidi hao?

a) ) Fafanua umuhimu wa anayerejelewa dondooni katika kukuza na kuendeleza vitushi riwayani. **(alama 4)**

b) Eleza sababu za mrejelewa kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari. **(alama 10)**

c) Mwandishi wa riwaya ya Nguu za Jadi amefanikiwa kutumia **mbinu ya majazi** katika kukuza wahusika na mandhari mbalimbali riwayani.Fafanua kwa kutolea mifano **sita**. **(alama 6)**

## SEHEMU D: USHAIRI

**Jibu Swali la 6 au 7**

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

<u>**Barabara.**</u>

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena,
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwa tayari kupanda na kushuka".

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka

Nipande na kushuka
Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendeleee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua,
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

***(Timothy Arege)***

**Maswali:**

(a) Taja aina ya shairi hili. **(alama 2)**
(b) Eleza toni ya shairi hili. **(alama 2)**
(c) Fafanua dhamira ya shairi hili. **(alama 2)**
(d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. **(alama 3)**
(i) Tanakuzi
(ii) mbinu rejeshi
(iii) Taswira
(e) Eleza umuhimu wa maswali balagha katika shairi. **(alama 2)**
(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. **(alama 4)**
(g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili. **(alama 2)**
(h) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 3)**

**AU**

***7. Soma shairi hili kisha uyajibu maswali;***

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo unayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo?
Kwacho, lijalo nalije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tusikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge yawakutayo,
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanatumuliya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaumiya, na mafia wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
Hawa, huwapa unene, watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waitikayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo.
Naandika!

**Maswali**

a) Malenga wa shairi hili alidhamiria kufafanua masuala kadhaa yanayokumba Jamii.Taja **manne** ya masuala haya kwa kurejerea shairi. **(alama 4)**

b) Tambua bahari za shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; **(alama 4)**

i) vina
ii) kibwagizo
iii) idadi ya vipande
iv) mishororo

c) Kwa kutoa mifano,tambua mbinu **mbili** ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. **(alama2)**

d) Tambua kwa mifano mbinu **mbili** za kimtindo alizotumia mshairi. **(alama4)**

e) Andika ubeti wa **nne** katika lugha nathari. **(alama 4)**

f)Tambua na ueleze toni katika shairi hili. **(alama 2)**

**SEHEMU E: HADITHI FUPI**

**D.Lutomia na Phibbian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

8***.Fadhila za Punda***

Alipozidiwa akapoteza fahamu.Fahamu zilipomrudia,maumivu yakamvamia.Mumewe hakuonekana,amejiendea na kumwaacha afilie mbali.Alilia machozi yakamwisha.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b)Taja mbinu **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Fafanua mbinu **nne** za kutambua sifa za mhusika anayerejelewa. **(alama 4)**

d)Kwa kurejelea hadithi "Fadhila za punda" onyesha kwa hoja **nane** ufaafu wa mdokezo wa methali ufuatao: ***maskini akipata makalio hulia bwata*** kwa kutolea mifano mwafaka hadithini. **(alama 8)**

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 9

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA**……………………………………………………………………………………

**SHULE**………………………………………………  **SAHIHI**…………………………

**INDEX NO**……………………………………………  **NAMBARI**………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

- *Andika insha mbili.*
- *Insha ya kwanza ni ya lazima.*
- *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
- *Kila insha isipungue maneno **400**.*

| SWALI | TUZO |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |
| 4 | |
| JUMLA | |

## MASWALI

**1.** Ndugu yako ameamua kuasi ukapera. Andika ratiba itakayotumiwa siku ya arusi yake.

**2.** Eleza mikakati ambayo serikali ya Kenya imeweka kukabiliana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Kigaidi nchini.

**3.** Andika insha kuonyesha busara iliyomo katika methali “Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe”.

**4.** Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:

**…**Nilikumbuka ushauri niliopewa na mama mazazi mara kwa mara. Uchungu usiomithilika ulinichoma moyoni, laiti ningalijua.

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 9

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**
**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE………………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO…………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO**

- ✓ *Karatasi hii ina sehemu nne. Ufahamu, Ufupisho, matumizi ya lugha na Isimu jamii.*
- ✓ *Jibu maswali yote katika nafasi uliziachiwa.*

**KWA MATUMIZI YA MUTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| UFUPISHO | 15 | |
| MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

***<u>Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali yanavyofuata</u>***

Wakati wananchi katika kila pembe ya dunia waliadhimisha siku ya wapendanao maarufu kama "Valentine Day," kwa mitindo mbali mbali, hali hiyo ilikuwa tofauti kwa baadhi ya wanaume nchini Kenya, baada ya kulalamika kuhusu kunyanyaswa na wake zao.

Kulingana na mwenyekiti wachama cha kutetea haki za wanaume nchini, idadi ya wanaume wanaopigwa na wake zao imeongezeka mno. Alisema juzi kuwautafiti wa chama chake umeonyesha kuwa harakati za kumpa mwanamke uwezo zimeathiri maadili na kusababisha kuwadharau wanaume. Mwanaharakati huyo alidai kuwa tatizo hilo limechochewazaidinahaliyakuwawanawakewengisasawanakipatokikubwakulikowaumezao.

Mwisho niwa mwezi polisi walimtia mbaroni mwanamke mmoja mjini Nyeri, baadaya kumshambulia mumewe na kumjeruhi kwa panga. Mwanamme huyo bado anapata matibabu hospitalini. Yeye alirudi nyumbani kama amevaa miwani ndipo akakatwa katwa usoni na uchunguzi kuhusu tukio hilo bado unaendelea.

Inadaiwa kuwa Zaidi ya wanaume 460,000 walinyanyaswa na wake zao mwaka jana na kwamba utafiti wa shirika la kuwatetea wanaume umeonyesha kuwa kesi nyingi za wanaume kuteswa na wake zao zina ripotiwa katika kati mwanchi.

Hata hivyo, baadhi ya wanaume katika eneo hilo wameunga mkono hatua ya wanawake kuwashambulia waume zao. Wanasema kuwa wanapigwa kwa sababu wamekosa kuwajibika kwa familia zao. Wanadai kuwa wanaume wengi <u>hawajulikani nyumbani kwao</u>. Wake zao wanawajua makasisi ambao hujakuwa ombea kuhusu matatizo ya nyumbani huku mabwanazao wakizama katika ulevi. Wanawake na waume wa Nyeri wametaka serikali kukomesha uuzaji na unywaji wa pombe haramu ambayo imechangia sana katika ugomvi wanyumbani.

## MASWALI

**a)** Yape Makala haya anwani inayofaa **(alama 1)**

**b)** Eleza sababu za wanaume kupigwa na wanawake katika ndoa **(alama 4)**

**c)** Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa wanaume wengine hawajulikani nyumbani kwao? **(alama 2)**

**d)** Fafanua majukumu ya makasisi katika jamii kwa mujibu wa kifungu hiki **(alama 2)**

**e)** Ni mabadiliko yepi yametokea katika asasi ya ndoa kwa mujibu wa kifungu**?** **(alama 3)**

**f)** Eleza maana ya msamiati kamaulivyotumikakifunguni **(alama 3)**

**i)** Mwanaharakati

**ii)** Amevaa miwani

**iii)** Waliadhimisha

## 2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo linalo wasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kuwa itapatika na leo au karne baadaye.

Yamkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhanaya ”Ujambazi” tena “wakimataifa”. Hili ni tatizo moja wapo nayapo mengi sana. Tatizo la pili ni kibusi. Kuna wale wafu binafsi na hasa viongozi wanchi kubwa kubwa na serikali zaozilizo jiamini shakuwa ujambazi nibalaa kweli, tena belua, lakini huoni wahuko, wala hauwezi kuwagu sa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni ya watakaburi hao, ujambazi ni wa watu washenzi wasio starabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi wapekee wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wadawa za kulevya iliosababishwa navinyangarika kutoka nchi hizo maaluniza “ulimwengu watatu”. Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa waustaarabu ulimwengu na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusagwa sagwa, ulimwenguni mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhi ni itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi, hata hivyo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba terehe kumi na moja, mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilizo elekea katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wazaidi yaghorofa mia moja na kuya twangi lia mbali. Mstuko na kimako! Kimako kwa kuwa kabla ya siku hiyo, wa marekani hangeweza kudhani kwamba ingeweze kamataifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kuishambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe yoyote ya dunia.

Hakuna ulimwengu mzima, aliyeamini kuwa marekani ingewezakushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko ulitingisha ardhi yote na huzuni kutanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, walasiomarekanipekee.

Mintarafu hiyo ,marekani ilipo lipiza kisasi kwa kuwa unguza

Walio kuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusheherekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pachaya New York naileya Pentagon, utiwa uwezo wa Marekani ilizorota. Kuna wengi waliodhani huoni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa nima jambazi wa kimataifa.

## <u>MASWALI.</u>

**a)** Bila kubadilisha maana, fupisha aya za kwanza.(maneno 65-70) **(alama 6)**

**Matayarisho**

**Jibu**

**b)** uKizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyo tendeka baadaya Septemba 11,2001.( maneno65-70) **( alama 7)**

**Matayarisho**

**Jibu**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(alama 40)**

**a)** Eleza sifa mbili bainifu za sauti /a/ **(alama 2)**

**b)** i) Mofimu ni nini? **(alama 2)**

**ii) Ainisha** mofimu katika kitenzi; **(alama 2)**

Alimwona

**c)** Andika kitenzi chenye muundo ufuatao; **(alama 2)**

Kiambishi ngeli, wakati uliopita, mzizi, kauli tendwa na kiishio.

**d)** Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha matumizi ya kiimbo. **(alama 2)**

**e)** Ziandike upya sentensi kulingana na maagizo yaliyo banwa. **(alama 4)**

**i)** Kijitabu kile kulirushwana kiranja. (Tumia kivumishi kisisitizi cha karibu)

**ii)** Barabara nyingi zimesakafiwa. (Tumia wakati ujao hali ya mazoea)

**f)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi **(alama 4)**

Cherotich aliwahakikishia wazazi wake kwamba angetia bidii katika masomo yake iliapite mtihani wake

**g)** Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia rejeshi-amba **(alama 2)**

**i)** Mshukiwa alipelekwa mahakamani

**ii)** Mshukiwa alichukuliwa hatua

**h)** Changanua sentensi ifuatayo kwa mtindo wa jedwali **(alama 4)**

Mto uliofurika mwaka jana uliwaua mamba wengi

**i)** Tambua shamirisho, chagizo nakihusishi katika sentensi **(alama 3)**

Mgonjwa alitibiwa na daktari jana jioni.

**j)** Taja ngeli za nomino zifuatazo **(alama 2)**

i) Sandarusi …………………………………………

ii) Saa………………………………………………….

**k)** Yakinisha sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mamlaka makubwa ya Rais haya kwa zijuhudiza upinzani

**l)** Unda nomino mbili kutokana na kitenzi kifuatacho **(alama 2)**

La

**m)** Tunga sentensi kudhihirisha maana za vitate vifuatavyo **(alama2)**

**i) Bure**

**ii) Pure**

**n)** Andika katika hali ya ukubwa wingi (**alama 2)**

Msichana mrembo ameolewa na mwanamume hodari.

**o)** Kamilisha tanakali za sauti zifuatazo **(alama 2)**

i) Maji yalijaa………………………………………………………………………………………

**p)** Barabara imenyooka Eleza maana ya mzizi wa kitenzi **(alama 1)**

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**a)** Lugha rasmi ni nini? **(alama 2)**

**b)** Eleza sababu zozote tatu ambazo huenda zikamfanya mzungumzaji afanye makosa ya kisarufi na kimatamshi **(alama 3)**

**c)** Huku ukitoa mifano mwafaka fafanua sifa tano za sajili ya bungeni. **(alama 5)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 9

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

**MAAGIZO:**

1) *Jibu maswali **Manne** pekee.*
2) *Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.*
3) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
4) *Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**
**SWALI LA LAZIMA**
**1.**
Ndimi kisoi, dume la ukoo mtukufu wa kifalme.
Ukoo wa kipekee, utukukao kwao ubingwa
Ubingwa wa kucheza ngoma
Uhodari wa kusakata rumba
Hakuna abishanaye name, uwanjani
Mabinti wang'ang'ania kusakata name
Bingwa kisoi aingia nyanjani

Soma kifungu kilicho hapo juu kisha ujibu maswali yafuatayo.
**a)** Tambulisha kipera cha maghani kinachojitokeza katika kifungu hiki. **(alama 2)**
**b)** Kipera ulichotaja katika (a) ni cha utanzu upi? **(alama 1)**
**c)** Fafanua sifa tano za kipera hiki. **(alama 5)**
**d)** Fafanua umuhimu wa kipera hiki. **(alama 2)**
**e)** Ngomezi ni nini? **(alama 2)**
**f)** i) Fafanua dhima tano za ngomezi. **(alama 5)**
ii) Taja mifano yoyote mitatu ya ngomezi za kisasa. **(alama 3)**

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA**
**Jibu swali la 2 au 3**
**2.** "Sisi tuna bahati ya mtende mtoto kutusikiliza na kutupiga jeki."
a) Tambua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
b) Kwa kutoa mifano minne, eleza vipi mrejelewa amewapiga jeki. **(alama 4)**
c) Taja na ufafanue mbinu iliyojitokeza katika dondoo. **(alama )**
d) Fafanua sifa sita za mnenewa. **(alama 6)**
e) Tambua na ufafanue maudhui yoyote mawili yanayojitokeza katika dondoo. **(alama 4)**

**3. a)** Kwa kurejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha, eleza namna mwanamke alivyosawiriwa. **(alama 10)**
b) Angazia kwa mifano mwafaka namna ambavyo maudhui ya utu yanavyojitokeza katika tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

**SEHEMU YA C: RIWAYA YA NGUU ZA JADI**
**Jibu swali la 4 au 5**
**4. a)** Riwaya ya Nguu Za Jadi ni kioo cha nchi za Afrika. Fafanua. **(alama 20)**
**5. …..** alifanya kazi yake kwa moyo wa kujituma. Hakunung'unika pale kazi zilipomzidi bali alitabasamu na kuchapa kazi. Matatizo ya nyumbani yalipomzonga, hakukosa kufika kazini. Alidunduiza vijisenti vichache ambavyo alikuwa akipokea kama ujira wake akaweza kuwasomesha wanawe.
a) Tambua muktadha wa dondoo. **(alama 4)**
b) Fafanua sifa nne za msemewa. **(alama 4)**
c) Jadili changamoto za kikazi zinazojitokeza katika riwaya ya Nguu Za Jadi. **(alama 12.**

**SEHEMU YA D: HADIDHI FUPI: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

**Jibu swali la 6 au 7**

**Harubu ya maisha na Paul Ng'ang'a Mutua**

6. Muda si mrefu, chakula kilikuwa tayari. Nilimlisha Mercy. Akalala. Akaniachia mzigo wa kupambana na njaa yangu mwenyewe. Lakini mtu anawezaje kula chakula mkewe akiwa njaa, tena hapo hapo katika chumba kimoja? Na kuongeza msumari wa moto kwenye kidonda kibichi, chakula kina harufu na muonjo wa mafuta taa! Hii kweli ndiyo maana ya kila msiba kuandamana na mwenziwe! Nilishindwa kula kabisa. Niliangalia mahali anakoweka sukari Mama Mercy. Mkebe ulikuwa shinda. Nilihisi machozi yanayotunga kwenye ncha za macho lakini nikajikaza kiume.

**a)** Tambua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
**b)** Tambua mbinu zozote zinazojitokeza katika dondoo. **(alama 6)**
**c)** Tambua maudhui yanayojitokeza katika dondoo. **(alama 2)**
**d)** Eleza sifa na umuhimu wa msimulizi. **(alama 6)**
**e)** Kwa kurejelea dondoo eleza maana ya kauli "msiba kuandamana na mwenziwe." **(alama 2)**

(Mzimu wa kipwere na Yussuf Shoka Hamad.)

**7.** ……….. mara nilisikia sauti ya mtu ikiimba ule wimbo wa mzimu ikiashiria kuomba ruhusa ya kuingia, kusikia vile, nikajua sasa nitafumaniwa na wahusika na bila shaka nitakabiliana na hukumu ambayo sitasahau milele iwapo nitatiwa nguvuni. Kwa kuhofia kupatwa na mnadhaa au idhara, nikaizima tochi yangu, tap! Kisha bila ya kupepesa macho mara mbili, nikajivurumisha uvunguni mwa kile kitanda chenye matendegu marefu kama miguu ya punda kirongwe nikakaa kimya na kutulia kama ninyolewaye! Wale watu wawili waliimba wimbo wao wa kawaida. Mara tu walipomaliza na kutambuana, wote waliingia mle ndani ya mzimu. Siku hii kama kawaida, walioingia mle mmoja alikuwa mwanamke na mwingine mwanaume. Bila ya kupoteza muda, Yule mwanaume alianza kwa kusema kwa sauti ambayo niliitambua kuwa ya Salihina. Hapo masikio yangu yalivuka kichwa kwa kumwogopa bwana yule aliyetisha sana, yakawa kama masikio ya sungura anayeiba mazao shambani.

**a)** Mwandishi katika kifungu hiki ametumia mbinu ya ulinganisho kwa mapana. Tambua mbinu hii na utaje mifano yoyote mitatu. **(alama 3)**
**b)** Tambua mbinu nyinginezo za lugha zinazojitokeza katika kifungu. **(alama 4)**
**c)** Fafanua sifa zozote tano za Salihina kama zinavyojitokeza katika hadithi ya Mzimu wa Kipwerere**.** **(alama 5)**
**d)** Fafanua umuhimu wa msimulizi. **(alama 2)**
**e)** Eleza umuhimu wa mandhari ya Mzimu wa Kipwerere. **(alama 6)**

**SEHEMU YA E: USHAIRI**

***8. Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Wanafunzi sikilizeni, niwape wangu wasia
Mkiwa mtihanini, muweze kuzingatia,
Nataka mtambueni, msije mkajutia
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Kufanikiwa kitaka, watii nao walimu
Sielekeze dhihaka, kwao wao ni muhimu,
Kwauliza mwahitajika, maswali yalo magumu,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mrauke na mapema, msome kwa tumaini,
Msije nyie kukwama, kwenye wenu mtihani,
Muweze rudia vyema, mlofunzwa awalini,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu,

Umoja ni nguvuni, mwafaa mfahamuni,
Jiunge na makundi, masomo mujadilini,
Na lile lilo gizani, takuja kulionani,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Ilopita mitihani, kwa chudi irudieni,
mpate na taswirani, ya ule ulo mwishoni,
Ya ziada kazini, ifanye sizembeeni,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mwelewe sana vyema, yaliyo mtaalani,
Msije mkandama, cha mtihani chumbani
Mgongeni ndipo vyema, sije mkapoteani,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mkiwa madarasani, kelele muepukeni,
Sije mkapotezani, muda wenu masomoni
Neneni na vitabuni, vitakuja walipani,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Michezo sipuuzeni, kwayo nyie burudika,
Nishati mtapatani, kifurahia michezo,
Mazoezi eleweni, ni muhimu kwa ubongo,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Nimefika kaditama, kuwelekeza moyoni,
Yafwateni hayo mema, mfaulu mtihani,
Ni upuzi msiseme, muda wangu potezeni
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

**a) Eleza** mawaidha yanayotolewa kwa wanafunzi kuhusu namna ya kujitayarisha vyema kwa mtihani. **(alama 5)**
**b) Eleza** umbo la shairi hili. **(alama 4)**
c) Eleza mbinu tatu zilizotumiwa katika shairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. **(alama 3)**
d) Taja mifano ya tamathali mbili zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 4)**
e) Eleza toni ya shairi. **(alama 1)**
f) Andika ubeti wa pili kwa lugha tutumbi/ nathari. **(alama 3)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 10

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**
**MUDA: SAA 1¾**

JINA…………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………

INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)*

## MAAGIZO

1. *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
2. *Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.*
3. *Kila insha isipungue **maneno 400***
4. *Kila insha ina **alama 20***
5. *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

## KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

## MASWALI

## LAZIMA

**1.** Wewe kama rais umekerwa na kukithiri kwa ufisadi katika wizara mbalimbali. Andikia arifa mawaziri wako ukiwaeleza madhara ya ufisadi na hatua utakazochukua ikiwa hawatakomesha ufisadi katika wizara zao. **(alama 20)**

**2.** Dhuluma katika asasi ya ndoa haiathiri tu wanajamii husika nyumbani bali elimu ya watoto wao pia. Fafanua. **(alama 20)**

**3.** Andika kisa kinachoafiki methali:…. Usishindwe kupika ukasingizia jiko la moshi. **(alama 20)**

**4.** Andika insha itakayokamilika kwa maneno yafuatayo:

**...**Ni jicho gani lisilolengwalengwa na chozi la mshangao na huzuni kwa kushuhudia unyama wa aina hii. Wanadamu wamesahau kuwa mtu ni utu**.** **(alama 20)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 10

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**
**MUDA: SAA 2½**

**JINA**………………………………………………………………………………

**SHULE**……………………………………………… **SAHIHI**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **NAMBARI**………………………

***Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)***

**MAAGIZO**

1. *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
2. *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
3. *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | JUMLA | |

## 1. UFAHAMU: (ALAMA 15)

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia.</u>***

Mawasiliano ni upashanaji habari kwa namna tofautitofauti. Njia za mawasiliano zimebadilika sana katika historia ya binadamu. Kwa mfano, zamani ingechukua siku nyingi kupitisha ujumbe baina ya watu wanaoishi sehemu mbalimbali. Siku hizi ujumbe hupitishwa katika sekunde chache katika masafa marefu.

Ugunduzi wa simu uliofanywa na Alexander Graham Bell mwaka wa 1876 ulifungua ukurasa mpia katika mawasiliano. Nchini Kenya, miaka ya sabini na themanini, ilikuwa vigumu kupata huduma za simu. Mtu alihitajika kusafiri masafa marefu ili kupata huduma hizo hasa kwa wale walioishi mashambani. Aidha kutokana na ukosefu wa huduma hizo katika sehemu nyingi, mtu alihitaji **kupiga foleni** ili ahudumiwe ama ajihudumie.

Baadaye, simu tamba zilivumbuliwa na mawasiliano yakarahisishwa. Mwanzoni, simu tamba zilikuwa vidude vikubwa ambavyo havikutoshea mifukoni. Hata hivyo, usumbufu huo ulitafutiwa suluhu. Siku hizi simu tamba ni ndogo na hivyo huwa rahisi kuzibeba. Aidha, kampuni za kutoa huduma za mawasiliano na kufanya gharama ya kupiga simu kuenda chini.

Barua pia ni njia ya mawasiliano na imetumika kwa muda mrefu. Baadhi ya nchi kuliko tumiwa barua katika enzi za zamani ni Misri na Uyunani. **Matarishi** walitumwa kupeleka barua. Barua zilichukua muda mrefu kufikia aliyeandikiwa. Aidha kutokana na kwamba si watu wote waliojua kusoma na kuandika, wachache waliokuwa na maarifa hayo waliwandikia na kuwasomea. Katika enzi hizi matumizi ya barua yamepunguzwa kwa kiwango kikubwa na tarakilishi na simu tamba. Kwa kutumia tarakilishi unaweza kutuma barua pepe. Aidha, kwa kutumia simu tamba unaweza kutuma arafa.

Waajiri wengi hupendekeza wanaoomba kazi watume maombi yao kwa kutumia baruapepe. Njia hii huondoa uwezekano wa wanaoomba kazi kutumia ufisadi ili wapate kazi. Aidha, njia hii husaidia kutunza mazingira kwani karatasi hazitumiwi. Katika elimu tarakilishi zinatumiwa shuleni kufundishia hivyo kurahisisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Aidha, kupitia tarakilishi iliyotandawizwa ama kuunganishwa kwa mtandao, watu huweza kujuliana hali na kupashania habari mbalimbali kutoka pembe zote za dunia. Changamoto katika hatua hii ni ukosefu wa nguvu za umeme hasa mashambani. Aidha,gharama ya kununua tarakilishi ni kali mno hasa kwa mataifa yanayoendelea ikizingatiwa kuwa yana changamoto za kimsingi kama vile kutojua kusoma na kuandika, magonjwa na umaskini.

Vilevile, redio ni chombo muhimu ambacho huchangia sana katika mawasiliano. Kwa sasa, hiki ndicho chombo cha pekee kinachomilikiwa na karibu kila familia. Hali hii inachangiwa na ukweli kwamba kunazo redio ndogo ambazo hutumia betri. Chombo hiki huwapitishia matangazo na habari kuhusu yanayotendeka kutoka pande zote za ulimwengu. Redio hufahamisha, huburudisha na kuelimisha. Wizara ya Elimu imekuwa ikitumia redio kufundishia masomo mbalimbali hasa katika shule za msingi.

Nani asiyejua kuhusu runinga? Chombo hiki pia hutoa mchango mkubwa katika mawasiliano. Runinga hushirikisha hisi za kusikiliza na kuona, kwa hivyo mawasiliano yake hufanikiwa sana. Hata hivyo, ni asilimia ndogo ya watu ambao wanaweza kuimiliki kutokana na gharama yake na pia si wengi wanazo nguvu za umeme majumbani mwao.

Mwalimu ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii oyote. Ni dhahiri shahiri mwasiliano ni sehemu muhimu katika kuimarika kwa uchumi. Vile vile huwezesha watu kutangamana na kubadilishana mawazo. Binadamu si kama visiwa vinavyosimama peke yavyo. Binadamu huhitaji kutangamana na binadamu wengine katika maisha na kwa hivyo mawasiliano ni muhimu.

**a)** Eleza kini cha taarifa hii. **(al. 1)**
**b)** Toa sababu mbili za waajiri kuhimizi matumizi ya barua pepe. **(al. 2)**
**c)** Kwa nini redio ndicho chombo kinachotegemewa zaidi katika mawasiliano. Eleza sababu nne. **(al. 4)**
**d)** Kwa mujibu wa kifungu hiki eleza udhaifu wa tarakilishi. **(al. 3)**
**e)** Eleza faida mbili za tarakilishi. **(al. 2)**
**f)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. **(al. 2)**
**i)** Kupiga foleni
**ii)** Matarishi

## 2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

**<u>Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo</u>**

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

**a)** Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)
**Matayarisho**
**Jibu**

**b)** Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho (Maneno 30) (alama 5 utiririko)
**Matayarisho**
**Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**a)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi viwili vya silabi moja. **(al. 2)**

**b i)** Eleza maana ya sauti za likwidi. **(al. 1)**

**ii)** Toa mifano ya sauti za likwidi. **(al. 1)**

**c)** Ainisha mofimu: Lililoliwa **(al. 3)**

**d)** Eleza huku ukitoa mifano matumizi mawili ya kiambishi 'ji'. **(al. 2)**

**e)** Huku ukionyesha upatanisho wa kisarufi katika sentensi, weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka. **(al. 2)**

**i)**Uwele

**ii)** Vita

**f)** Tumia 'O' rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo. **(al. 1)**

Tawi limekauka

Tawi limeanguka

**g)** Tambua vivumishi na uonyeshe ni vya aina gani. **(al. 3)**

Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu.

**h)** Kanusha: Msichana ambaye amefika ametuzwa. **(al. 1)**

**i)** Onyesha aina za virai katika sentensi hii: **(al. 2)**

Wale wazazi wetu watawasili kesho saa tatu.

**j)** Unda nomino kutokana na kitenzi 'Haribu' **(al. 1)**

**k)** Tambua aina za vitenzi katika sentensi. **(al. 2)**

Hawa sio wachezaji bali wamekuwa wakichezea timu hii.

**l)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya viunganishi vya kulinganua. **(al. 1)**

**m)** Eleza matumizi mawili ya 'ka' . Toa mifano katika sentensi. **(al. 2)**

**n)** Andika visawe ya maneno yafuatayo **(al. 2)**

**i)**Daawa**……………………………………………………………………………………**

**ii)**Ainisha**………………………………………………………………………………**

o) Onyesha kwa kauli ulizopewa **(al. 1)**

**i)** Ja (tendewa)

**p)** Andika kinyume: Tajiri aliyesifiwa amelaaniwa. **(al. 1)**

**q)** Chananua sentensi hii kwa kutumia vishale. **(al. 4)**

Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo.

**r)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(al. 2)**

Oyula atapendwa na wengi ikiwa atashinda leo.

**s)** Eleza majukuma mawili ya chagizo huku ukitoa mifano. **(al. 2)**

**t)** Akifisha. **(al. 3)**

sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote kumbuka

**u)** Andika ukubwa wa sentensi katika wingi. Nyundo imo ndani ya kibweta. **(al. 1)**

## 4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**a)** **Eleza** matatizo matano yanayowakabili wazungumzaji wa Kiswahili. **(al. 10)**

# KCSE 2025 TOP SCHOOLS MOCKS

## JARIBIO LA 10

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI…………………………**

**INDEX NO………………………………………… NAMBARI………………………**

***Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(K.C.S.E)***

**MAAGIZO:**

***1)*** *Jibu maswali **Manne** pekee.*
***2)*** *Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.*
***3)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
***4)*** *Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU YA A: NGUU ZA JADI** **(ALAMA 20)**

**1. SWALI LA LAZIMA**

"Ndugu zangu, ukabila ni sumu ya nyoka. Ukabila huangamiza maendeleo ya nchi hata kama imestawi kiasi gani."

**a)** Yaweke maneno haya katika muktadha wake**.** **(alama 4)**

**b)** Eleza umuhimu nne wa msemaji wa kauli hii. **(alama 4)**

**c)** Onyesha mbili za uandishi zinazojitokeza katika dondoo hili**.** **(alama 2)**

**d)** Kwa kutumia hoja zisizopungua kumi, jadili maudhui ya ukabila yanavyojitokeza katika riwaya hii. **(alama 10)**

**SEHEMU YA B: BEMBEA YA MAISHA**

**JIBU SWALI LA 2 AU LA 3**

**2**. Wanasema kuwa Mungu hamtupi mja wake. Kweli iliyoje!

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Fafanua sifa za msemaji. **(alama 4)**

(c) (i) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. **(alama 6)**

(ii) "Lakini inakujuzu uelewe kuwa dunia ni nyumba ya mtihani." Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya *Bembea ya Maisha*. **(alama 6)**

**AU**

**3**. (a) ***Changanua mbinu za kimtindo katika dondoo lifuatalo***. **(alama 8)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (Kimya). Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (Kimya). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (Kimya). **Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya**. Maisha mapya. Pombe! (kama anayesemea pombe). Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu.

**(b)** Kauli iliyokolezwa wino katika dondoo inadokeza nia ya kubadilika kwa mzungumzaji. Kwa kurejelea tamthilia nzima, onyesha jinsi mwandishi alivyoshughulikia suala la mabadiliko.

**(alama 12)**

**SEHEMU YA C: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO**

**JIBU SWALI LA 4 AU LA 5**

**4. MSIBA WA KUJITAKIA** **(ALAMA 20)**

"Tayari alikuwa amefanya kosa. Kosa ambalo alifahamu lilikuwa la kujitakia."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Bainisha toni inayodokezwa na dondoo hili. **(alama 2)**

c) Hadithi ya *Msiba wa Kujitakia* ina matukio mengi yanayoonyesha kinaya. Thibitisha. **(alama 6)**

d)"Tamaa mbele mauti nyuma." Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi: Nilitamani. **(alama 8)**

**AU**

**5.** Jadili jinsi maudhui ya **usaliti** yanavyojitokeza katika hadithi zifuatazo: **(alama 20)**

- **i.** Toba ya Kalia
- **ii.** Kifo cha Suluhu
- **iii.** Fadhila za Punda
- **iv.** Mapambazuko ya Machweo

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

**6. SHAIRI HURU** **(ALAMA 20)**

***Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali***

Nimeyaandika maneno haya
Kwa niaba ya:
Mamilioni wasio malazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi
Wazungukao barabarani bila mavazi
... milki yao ya Maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
Wiki baada ya wiki
leo sumu au spaki
leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
Kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
kama kwamba sote tu vipofu,

Na kwa niaba yete sote;
Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni, machoni
Tuliotiliwa sumu, malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini
ili ‘maendeleo’
yaendelee kwenda njiani
huku yakitema machicha ya roho zetu.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Tetea jibu lako. **(alama 2)**

b) Bainisha toni ya shairi hili . **(alama 2)**

c) Tambua aina tatu za urudiaji zinazojitokeza katika shairi. **(alama 3)**

d) Huku ukitoa mifano eleza namna mtunzi alivyotimiza arudhi za kishairi. **(alama 3)**

e) Eleza matumizi ya.

i) Mistari mishata **(alama 1)**

ii) Mistari kifu **(alama 1)**

f) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. **(alama 2)**

g) Tambua aina za taswira katika shairi hili. **(alama 2)**

h) Mshairi anazungumza kwa niaba ya watu mbalimbali. Jadili.: **(alama 4)**

**AU**

**7. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali.***

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyahutubu
Wayasome ndugu zangu, wa mbali na karibu
Cha wenye raha na taabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, chenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kuta na kucha twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa *balaa*, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina, Saidi Ali Rajabu
Wengune kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenye dini, watiio Wahabu
Mashekhe misikitini, humo hufanya muhibu
Mapadri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa, na moyo *kisebusebu*
Tunakaribia kufa, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na mengine sitotaja, msinambe nina gubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

**Maswali**

**a)** Eleza mambo yanayojitokeza katika shairi hili. **(alama 3)**

**b)** Ainisha bahari katika shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(alama 3)**

(i) Mpango wa maneno

(ii) Vipande

(iii) Vina

**c)** Onyesha jinsi mbinu alizotumia mshairi kukidhi mahitaji ya kiarudhi. **(alama 3)**

**d)** Onyesha umbo la ubeti wa 3. **(alama 3)**

**e)** Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi **(alama 4)**

**f)** Mshairi huyu ni bingwa kwa kutumia lugha. Thibitisha. **(alama 2)**

**g)** Fafanua toni katika shairi hili. **(alama 1)**

**h)** Eleza maana ya neno ***kisebusebu*** kama lilivyotumiwa katika shairi **(alama 1)**

**8. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI** **(ALAMA 20)**

Mtoto wetu lala
Mtoto wetu lala
Mama ameenda sokoni
Kununua ndizi, atakuja na ndizi nyingi
Ndizi kubwa itakuwa yako
Utakula yote mtoto wetu
Kwa sababu mama anakupenda
Mama anakupenda
Mtoto wetu lala
Baba ameenda shambani kuvuna
Mimi mlezi wako nitakutunza kwa upendo
Nitakuandalia samaki kama jana
Mtoto wetu lala
Mama anakupenda sana.

**Maswali**

a) Huu ni wimbo wa aina gani. Thibitisha**.** **(alama 2)**

**b)** Taja na uthibitishe shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii asili ya wimbo huu. **(alama 2)**

c) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anaimbia nani**?** **(alama 2)**

d) Eleza mbinu ambazo mwasilishaji wa utanzu huu anaweza kutumia ili kufanikisha uwasilishaji wake. **(alama 2)**

e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii. **(alama 5)**

f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii **(alama 2)**

g) Umepewa wajibu wa kutafiti mbolezi katika jamii yako. Pendekeza mbinu ambazo ungetumia kutafiti kipera hiki. **(alama 5)**

# THE END

## FOR THE FOLLOWING;

- ONLINE TUITION
- REVISION NOTES
- SCHEMES OF WORK
- SETBOOKS VIDEOS
- TERMLY EXAMS
- QUICK REVISION KITS
- KCSE TOPICALS
- KCSE PREMOCKS
- TOP SCHOOLS PREMOCKS
- JOINT PREMOCKS
- KCSE MOCKS
- TOP SCHOOLS MOCKS
- JOINT MOCKS
- KCSE POSTMOCKS
- TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- KCSE PREDICTIONS
- KCSE REVEALED SETS

# *To Obtain Copies of Respective Marking Schemes / Answers*

# CALL/TEXT/WHATSAPP

# *0746-222-000*

# *0742-999-000*

*mwalimuconsultancy@gmail.com*

*This is a Copyright Property of Mwalimu Consultancy Ltd.*

# Powered By Mr Isaboke

# SUCCESS